# KISWAHILI FASIHI

# &

# USHAIRI

Mr Isaboke

(0714497530)

# FASHIHI SIMULIZI NA USHAIRI

**FASIHI SIMULIZI**

**.a) Eleza mbinu ambazo mtafiti wa fasihi simulizi hutumia katika kukusanya data ya fasihi simulizi**

- Mahojiano – kuuliza maswali na kujibiwa.
- Kinasa sauti – kihifadhi sauti au matendo.
- Uchunguzi – kishiriki kwa kufanya uchunguzi.
- Uandishi – kusoma makala mbalimbali juu ya jambo unalohitaji.
- Hojaji – kuandika hati ya orodha ya maswali ambayo humwongoza mtafiti katika utafiti.

Filamu na video – kamera huhifadhi sauti, mandhari n.k..

**Eleza usawa uliopo baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi**.

Fasihi andishi na fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutumia maneno yaliyofungwa vizuri yakavutia machoni, masikioni na nyoyoni.

- Zote huangaza mambo yanayotendeka katika jamii kwa mfano siasa, uchumi, elimu, na hata desturi
- Zote hutumia lugha ya kisanaa wala si lugha ya kawaida.
- Zote hutoa ujumbe maalumu kwa jamii.
- Zote hutungwa
- Zote huhifadhiwa kwa namna mbalimbali
- Zote zina tanzu zao
- Zote huwasilishwa kwa hadhira

Zote hurekebishwa panapotokea haja (mabadiliko ya wakati na mahitaji)

## NYISO

**b) Nyiso ni nini?** Nyimbo zinazohusishwa na jando au tohara .

c) **Fafanua sifa zozote nne za nyiso.**

**Sifa za nyiso**

- Kuonyesha utukufu wa jamii husika
- Huambatana na wakati maalum
- Zina msamiati unaoonyesha ujasiri
- Hazizingatii tasfida / heshima / adabu.
- Zingine huwa na sifa za huwatisha waoga
- Huorodhesha masharti ya kuvuka kutoroka

Rika / harua moja hadi nyingine .

### MIGHANI

a) **Maghani ni nini?**

- Maghani ni utungo wa kishairi ambao hutongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji..

**b)Eleza fani zifuatazo za maghani**

i)Vivugo -------**Vivugo** ni ushairi wa kujisifia unatungwa papo hapo na fanani mwanaume.
ii) Tondozi---- **Tondozi** – utungo wa kutukuza watu, wanyama, vitu kama magari, miti, milima n.k.
iii)Pembezi-- **Pembezi** – ni aina ya tondozi ambayo imekusudiwa kusifia watu na aina Fulani katika jamii kutokana na matendo yao au mchango wao katika jamii.
iv) Rara---- **Rara** – Ufungo wa kishairi wenye ubunifu mkubwa unaokusudiwa kusisimua hadhira.

**Sifa za maghani.**

i. Huwasilishwa kwa kalima.
ii. Huweza kuambatana na ala za muziki.
iii. Muhtasari/huwasilishwa kwa maneno na beti chache.
iv. Matumizi ya lugha ya kitamathali.
v. Ujumbe hujitokeza kwa mafungu ya mistari (beti)
vi. Kuwepo kwa kiongozi (mghani)
vii. Huhitaji mahali na wakati maalum.

Kuwepo kwa hadhira.

- **Dhihirisha tofauti ya kimsingi iliyopo baina ya maghani ya kawaida na yale ya masimulizi.**

-Maghani ya kawaida huwa mafupi na hushughulikia maudhui ya kawaida katika jamii kama vile: ndoa, elimu, mapenzi, siasa na maombolezi.

Maghani ya masimulizi huwa marefu na yanahusu masuala mazito kama vile dini, vita, wosia

**d) Taja na ueleze kwa ufupi vipera vyovyote vitatu vya maghani ya kawaida**.

i. Tondozi: Tungo za kuwasifu watu, wanyama au vitu (Tungo za sifa kwa jumla)
ii. Pembezi: Aina ya tondozi inayolenga kusifu watu maalum katika jamii kutokana na umuhimu au mchango wao kwa mfano: mashujaa, viongozi, n.k. (Tungo za kusifu binadamu/watu pekee).

Majigambo/vivugo. Tungo za kinudhuma ambapo watendaji hughani sifa zao./ Tungo za kinudhuma zinazotungwa papo kwa papo na kuwasilishwa kwa hadhira aghalabu na fanani mwanaume kwa nia ya kujisifu.

e) **Pendekeza hoja mbili kuonyesha dhima ya maghani katika jamii.**

i. Kuendeleza utamaduni wa jamii.
ii. Kuhifadhi matukio ya kihistoria.
iii. Kuhimiza watu wawe mashujaa kwa mfano majigambo.
iv. Kuleta umoja/ushirikiano baina ya watu katika jamii.
v. Kukuza vipawa.

## ULUMBI

**Eleza maana ya neno ULUMBI —** Uhodari wa kuzungumza au kuiga mazungumzo kwa usanii na uhodari mkubwa.

**Bainisha sifa za mlumbi**

**Sifa za mlumbi**

- Mwenye ujuzi wa utamaduni, desturi, mila na sheria za jamii (mzingiro) ujuzi mkubwa wa maisha
- Ufundi wa kutumia lugha, semi, mafumbo nk
- Uwezo wa kutumia mbinu mbalimbali za kuwasiliana mfano, nyimbo, ushairi
- Umahiri wa kughani, kusema kwa mfululizo na mwendo wa kasi
- Kutumia sauti inayosikika bila shida
- Ufundi wa kutumia kunga za maswali.

**Eleza umuhimu wa ulumbi**

**Umuhimu wa ulumbi**

-Kipimo cha kimsingi cha mtu kuteuliwa kama kiongozi
- Njia maalumu inayotumiwa na jamii kupitisha ujumbe muhimu
- Njia ya kudumisha utamaduni n thamani za kitamaduni kwa kuzionea fahari
- Ni kitambulisho muhimu kwa jamii na wanajamii.

# MISIMU

**Eleza maana ya**

**Misimu-- i) Misimu** – lugha ya kisirisiri yenye mafumbo itumiwayo na kundi ndogo la watu katika jamii.

**=Lakabu--- Lakabu** – majina ya kupanga au utani ambayo watu katika jamii hujipa au hupewa

**= ngomezi -- Ngomezi** – fasihi simulizi inayotumia ngoma au zana za kimuziki

=**Shauri mambo matatu anayopaswa kuzingatia mtu anapohitajika kufumbua fumbo**

i)ufahamu wa lugha iliyotumiwa km takriri, udogoshaji au ukubwa nk

ii)ufahamu wa mazingira, utamaduni na hali ya maisha ya watu. Hii ni kwa sababu mafumbo na majibu hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine.

iii)uwezo wa kupata jawabu kwa kulihusisha na mfanano wa hali, tabia au sifa Fulani zinazojitokeza katika kauli ya fumbo.

= **Fafanua umuhimu wa misemo**

i) Huogeza ladha katika mazungumzo kwa kupamba lugha.

ii) Huonyesha ustaadi wa lugha

iii) Hutumika kama tauria (ufunika ukali) km-kata kamba
- acha mkono
- kututoka

iv) Huchochea akili ya mzungumzaji au mzungumziwa

## NYIMBO

i) **Eleza maana ya nyimbo**

Ni tungo zilizoundwa kwa maneno ya kupendeza yaliyoteuliwa kiufundi, kiufasaha na yenye utaratibu wa sauti za kimuziki zinazopanda na kushuka.

ii) **Taja vigezo vinne muhimu vinavyotumiwa kuzipa majina aina mbalimbali za nyimbo.**

-Vigezo vinne.
- Umri wa wahusika
- Muktadha
- Jinsia
- Lengo la wimbo
- Zana zinazoambatana na wimbo

iii) **Eleza muundo wa nyimbo kwa jumla.**

-Hugawika katika beti
- Beti huwa na mistari
- Mistari huwa na silabi zenye mapigo ya kimuziki
- Baadhi ya nyimbo huwa na vina
- Nyingine huwa na kiitikio
- Mstari wa mkarara haubadiliki – mara nyingi ndicho kiini cha wimbo
- Waimbaji wana uhuru wa kubuni maneno na kuongezea kulingana na sherehe.
- Hutumia lugha inayoelezea mambo mengi kwa njia ya mkato/mafumbo

iv) **Fafanua umuhimu wa nyimbo za tahili katika jamii.**
- Huimbwa wakati wa maombolezi au kifo
- Hufichua hisia juu ya kifo
- Husifu waliofariki
- Hukashifu maafa
- Hufunza utamaduni unaohusiana na matanga

- Hujenga umoja katika jamii

Hutuliza nyoyo za waliofiwa.

## VITENDAWILI

a) **(i) kitendawili**

**Maana**

Aina ya usemi wa kimafumbo ambao hutolewa mbele ya mtu au watu ili wanaotakiwa kufumbua kwa kutoa jibu fulani. Fumbo hili huwa na umuhimu fulani kwa jamii inayohusika na sehemu muhimu ya chemsha bongo katika jamii hiyo

(ii) **sifa bainifu za vitendawili.**

**Sifa**

-Huwa ni vya aina mbalimbali za sitiari ambazo huchora au kujenga picha za kitu, mti, vitu, wazo dhana au hata maumbile fulani

-Mahali na wakati wa kutega na kutegua vitendawili hutofautiana kutoka jamii hadi jamii-vikao vya kutega na kutegua. Vitendawili vilikuwa jioni miongoni mwa watoto

-Vitendawili huwa na sifa fulani za kimuundo. Sifa kuu ni kwako kwa kifungu ambacho hutanguliza kila tendo la utegaji kitendawili. Mtegaji: Kitendawili

Msikilizaji: Tega

-Vitendawili hutumia lugha ya kimafumbo. Maana hufichwa ambayo msikilizaji anapaswa kutegua

-Umbo na maudhui ya vitendawili hudhibitiwa na hutegemea mazingira ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na hata kimaduni, kama km ni rahisi kujua jamii inajihusisha na amali au shughuli gani kutokana na vitendawili vyake

-Vitendawili huwa na sifa ya ufupi ya kimatizo. Vitendawili huweza kujengwa au kuundwa kwa kutegemea lugha ya ufananisho au ulinganisho kwa kinyume au alinganishe, lugha ya kitanakali au ya mwigo wa sauti

**(iii) umuhimu wa vitendawili katika jamii**

**Umuhimu wa vitendawili**

-Huelimisha-vitendawili huwa na msingi wa kuelimisha wanajamii kuhusu mazingira yao

-Kuburudisha-hutegwa na kuteguliwa katika vikao mbali mbali na huwa msingi wa burudani

-Kukuza uwezo wa kumbuka-Vitendawili huweza kutumiwa kupima na kudhamini uwezo wa wanajamii wa kuyakumbuka mambo

-Kuhifadhi historia ya wanajamii. Vitendawili ni nyenzo muhimu ya kuhifadhi historia ya jamii kwa kuonyesha imani zao, dini yao, elimu yao n.k

-Chemsha bongo

-Kuchochea udadisi-husaidia kujenga

**a) Eleza hatua zinazofuatwa wakati wa utegaji wa vitendawili?**

1Utangulizi – Mtegaji hutahadharisha hadhira iwe tayari kwa kitendawili kwa kuwatajia neno ‘kitendawili.’

2. Hadhira huonnyesha iko tayari kwa kijibu ‘tega’
3. Mtegaji anakitega kitendawili chake kwa hadhira.
4. Hadhira hutoa jibu la kitendawili walichopewa.
5. Jibu likipatikana mtegaji anakubali na natega kitendawili kingine.
6. Hadhira ikishindwa kupata jibu, wanampa mtegaji zawadi yaweza kuwa mji au msichana.
7. Akiridhika na zawadi/mji, anawapa jibu la kitendawili na kumpisha mwingine atoe kitendawili.

## MAIGIZO

**a) maana ya maigizo katika fasihi simulizi.**

Maigizo ni sanaa ambayo watendaji huiga matendo ya watu katika jamii, viumbe na

vitu vingine ili kuwasilisha ujumbe huku hadhira ikiburudika

b) **Taja sifa tano za maigizo katika fasihi simulizi.**

**Sifa**

i) - Hutendwa mbele ya hadhira maalum, ukumbuni
ii) - Kuna lugha ya picha
iii) - Kuna ufundi wa hali ya juu kama matumizi ya tamathali za usemi na mafumbo
iv) Kuambatana na aina nyinginezo za fasihi simulizi km nyimbo na ngoma
v) Uigaji hutegemea sauti na maleba
vi) Hutegemea matukio ya wakati huo ( maswala ibuka)
vii) Maneno huambatana na utendaji wa wahusika

**c) umuhimu wa maigizo katika fasihi simulizi.**

**Umuhimu**

i) Kukuza maadili
ii) Kuendeleza vipawa
iii) Kufunza watu kuhusu maisha
iv) kufurahisha au kujifurahisha ( hadhira)
v) Kuimarisha tamaduni na desturi za jaini
vi) Huboresha kufikirisha
vii) Huwezesha watu kudhibiti hisia zao
viii) Huwapa watu stadi mbali mbali na maarifa

**=Taja vitanzu vitatu katika kipera cha maigizo**

Vichekesho
(ii) Mchezo wa kuigiza
(iii) Majigambo
(iv) Ngonjera

## NGOMEZI

a) **Ni nini maana ya ngomezi**?

Ngomezi ni fasihi ya ngoma ambayo hutumiwa kupeleka ujumbe Fulani.

b) **Fafanua sifa tano za ngomezi?**

**Sifa za ngomezi:**

(i) Fasihi ya ngoma
(ii) Mapigo ya ngoma huwasilisha ujumbe maalum
(iii) Mapigo ya ngoma hufasiriwa kulingana na jamii husika.
(iv) Ujumbe wa mapigo ya ngoma hueleweka tu na watu kutoka jamii husika kwani kila jamii ina mapigo yake.
(v) Ni njia rahisi ya kuwasilisha ujumbe mzito/maalum.
(vi) Mapigo huwa mahsusi kulingana na jamii kama zilivyo tungo nyingine za fasihi simulizi.
(vii) Ujumbe unaowasilishwa huweza kufichwa kwa wasiohusika.

## MISIMU

6. a**) Eleza maana ya misimu.**

i) Misimu ni maneno yanayozuka na kutumiwa katika mazungumzo na makundi maalum ya watu katika jamii.

Maneno haya hatimaye hupotea na machache yanayodumu husanifishwa na kuwa msamiati rasmi wa lugha.

c) **Eleza sifa sita za misimu**.

(i) Huzuka na kutoweka baada ya muda k.m mambo bado, jaajaa, dunda.
(ii) Baadhi ni maneno yasiyo sanifu k.m ushago, mahewa, utadoo.
(iii) Ni Lugha ya mafumbo k.m waya, machozi ya simba, kuwaka, mbao.
(iv) Maneno huwa na maana nyingi k.m mahewa kwa maana ya muziki, uongo au ulevi wa madawa
(v) Baadhi ya maneno huweza kuingizwa katika lugha sanifu k.m matatu, bodaboda,chokoraa, mdosi
(vi) Maneno hugawika katika makundi mbalimbali k.mmisingi ya vijana,walevi, wanajeshi, jambazi, usafiri,mavazi

**a) Ainisha tanzu zozote tatu za mazungumzo**

Hufanywa kati ya watu juu ya jambo Fulani na huwasilishwa kwa kusemwa kifasili.

**Malumbano ya utani -** Mazungumzo ya kufanyiana mzaha au masihara
**Soga** – mazungumzo ya kupitisha wakati na hulenga kuchekesha, kukejeli, kukebehi watu au hali fulani.
**Mawaidha** – maneno mazuri, ushauri au maonyo
**Ulumbi** – usemaji wa ufasaha na madoido unaolenga jambo Fulani

**b) Ni kwa nini watu hupewa au hujibandika majina ya lakabu?**

kutoa sifa mbaya na kukejeli wahusika wabadilike

- Hutokana na sifa au hulka aliyo nayo mtu k.m. Simba wa Yuda
- Zingine hutiwa chumvi – Malkia

# MASWALI NA MAJIBU YA FASIHI

## 1

a) Fafanua sifa tatu za kila mojawapo ya vipera vya fasihi simulizi vifuatavyo (alama6)
  i) Vitendawili
  ii) Methali
b) Mawaidha yana dhima gani katika jamii? Eleza (alama6)
c) Bainisha sifa za nyimbo. (alama4)
d) Eleza umuhimu wa nyimbo za kisiasa (alama4)

**MAJIBU**

**SIFA ZA VITENDAWILI**

Sifa za vitendawili

i) Huhusisha makundi mawili ya watu – mtegaji na mteguaji
ii) Huwa ni fumbo au mseto wa mafumbo
iii) Hutumika kama chemsha bongo
iv) Maana yake hueleweka katika jamii husika tu
v) Huwa na funzo maalumu kwa washiriki (hadhira)
vi) Hutambwa wakati maalumu/teule
vii) Vina muundo wa kipekee katika utangulizi: Mtegaji husema “Kitendawili” na mteguaji huitikia “tega.”
viii) Fanani/ mtegaji hudai zawadi (mji) hadhira inaposhindwa kutegua.

**ii) SIFA ZA METHALI**

i) Huwa fupi – maneno huwa machache
ii) Kuna matumizi ya ukariri k.m. haraka haraka haina baraka
iii) Zinaeleweka katika muktadha teule
iv) Hufuata mtindo wa kimafumbo
v) Huwa na ufanano wa kimaana
vi) Zina ukinzano wa aina Fulani k.v. Ukupigao ndio ukufunzao.
vii) Hulinganisha mambo na hali k.v. lisilokuja asubuhi, lingoje jioni

viii) Hutoa mafunzo mahsusi

b**) DHIMA YA MAWAIDHA**

i) Huelimisha
ii) Huwa kama kielelezi kwa jamii
iii) Huwatia watu changamoto hasa za kuchanganua mambo na hali mbalimbali katika jamii.
iv) Nimsingi wa kuiandaa hadhira kupambana na matatizo ya maisha
v) Hustawisha na kuendeleza utamaduni ufaao katika jamii
vi) Hukuza na kuendeleza ushirikiano katika jamii

c**) SIFA ZA NYIMBO**

i) Huimbwa na mtu mmoja au kundi la watu
ii) Huimbwa na kuambatana na kucheza
iii) Huandamana na ala za muziki kama ngoma
iv) Waimbaji hujipamba kwa mavazi maalum
v) Hubeba ujumbe mzito
vi) Hulingana na majira mbalimbali
vii) Hugusa hisia za watu kwa njia mbalimbali
viii) Waimbaji huwa na sauti za kipekee zinazotolewa kwa mahadhi au rithimu fulani.

**d) UMUHIMU WA NYIMBO ZA KISIASA**

i) Husifu viongozi na uongozi wao
ii) Hukashifu uongozi mbaya/usiofaa
iii) Huwazindua watu kupigania haki zao
iv) Huhamasisha watu kutekeleza jambo fulani
v) Huonyesha hisia za uzalendo
vi) Huonyesha utesi juu ya kunyanyaswa

**SAWALI 2**

. (a)Eleza namna ambavyo hadhira wanahusishwa katika utambaji. (alama 8)
(b) Taja sifa nne bainifu za hadithi. (alama 4)
(c) Fafanua sifa nne za fanani/mtambaji bora. (alama 8)

## <u>jibu</u>

**a) –** Kuulizwa kutoa mafunzo ya hadithi
•Kuimba
•Kuchekeshwa
•Kuulizwa maswali yanayoilenga hadithi
•Kukamilisha sentensi za mdokezo 2 x 4 = 8
b) – Hutumia lugha elezi
- Hufunza maadili fulani katika jamii
- Huwa na mwanzo na vimalizio maalum
- Hubeba utamaduni wa jamii husika. ***2 x 4 = 8***

**3**

1. a) Maghani ni nini? (alama2)
b) Eleza fani zifuatazo za maghani. (alama8)
i) Vivugo
ii) Tondozi
iii) Pembezi
iv) Rara
c) Eleza maana ya neno <u>Ulumbi</u> (alama2)
d) Bainisha sifa za ulumbi. (alama8)

# jibu

1. (a) Maghani ni utungo wa kishairi ambao hutongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji (alama 2)

(b)

(i) Vivugo ni ushairi wa kujisifia unoatungwa papo kwa hapo aghalabu na janani mwanaume.

(ii) Tondozi - utungo wa kutukuza watu, wanyama vitu kama magari, miti, ng'ombe, milima nk.

(iii) Pembezi - ni aina ya tondozi ambayo imekusudiwa kusifia watu wa aina fulani katika jamii kutokana na matendo yao au mchango wao katika jamii.

(iv) Rara: Ni utungo wa kishairi wenye ubunifu mkubwa unaukusudiwa kusisimua.(Hoja4 x 2 = 8)

(c) Uhodari wa kuzungumza au kuiga mazungumzo kwa usanii na uhodari mkubwa (alama2)

(d)

- Ujuzi wa kina wa utamaduni, desturi, mila na sheria za jamii
- Mzingiro mpana wa maisha
- Ufundi wa kutumia lugha, semi, mafumbo n.k.
- Uwezo wa kutumia mbinu mbali mbali za kuwasiliana mfano, nyimbo, ushairi n.k.
- Umahiri wa kughani, kusema kwa mfululizo na mwendo wa kasi.
- Kutumia sauti inayosikika bila shida.
- Ufundi wa kutumia kunga za maswali

**SAWALI 4**

a) Methali ni nini? (alama2)

b)Ainisha sifa Tano za methali za Kiswahili (alama10)

c) Elezea umuhimu wa hadithi kama utanzu wa fasihi simulizi katika jamii (alama8)

# jibu

(a) **Maana ya methali**

Ni semi fupi zenye maana fiche ambazo zinatumika kufafanua mambo na hekima katika jamii. Methali hutumika kutolea mifano (mithilisha) mambo, tabia, matendo au matukio fulani katika maisha ya jamii. Hufanya hivyo kwa maelezo ambayo yamefupishwa na si bayana lakini yaliyo na maana pana

(b) Sifa za methali

(i) Huwa na sehemu mbili. Maana ya nje na ya ndani.k.m. ***Kila mwamba ngoma ngozi huivutia kwake.*** Anayewamba ngoma- sharti avute ngozi kujielekea ili aweze kuikaza vyema. Kila jambo zuri linapotokea watu hutaka kujihusisha nalo, kuonekana ndiwo waliolifaniksha

(ii) Lugha yao hudhihirisha ukale na usasa wa jamii inayozitumia. Methali za zamani hutumia msamiati wa kale. K.m. ***Mkata hendi mkele, na angenda mkele akipakia jahazi mteletele, hurudi na upele***. Vile vile kuna methali ya kisasa. Kula uhondo kwataka matendo, asiye na matendo hula uvundo

(iii) Huwa na muundo maalumu. Hujigawa vipande viwili kama mshororo katika shairi. Kipande cha kwanza hutoa wazo au pendekezo cha pili kikijibu au kutoa mwelekeo wake. Mfano: fimbo ya mbali (wazo/ pendekezo), haiui nyoka (jibu). Mtoto akililia wembe (pendekezo/ wazo), mpe (jibu)

(iv) Hubadilika kulingana na jinsi lugha ya jamii inavyokua. Mfano kazi mbi si mchezo mwema

(v) Hudhihirisha ujuzi wa mtumizi wake. Hutumika kutolea maudhui au mafunzo kwa, njia ya mafumbo.

Mficha uke hazai

(vi) Huwa na mapigo ya kishairi. Mpangilio wa maneno yake huwa na mbinu za kishairi. Mfano;

Maskini akipata, matako hulia mbwata

Asiyekuwapo, na lake halipo

(vii) Msamiati teule hufunza fani za lugha

Mfano:

Haba na haba hujaza kibaba (takriri)
Haraka haraka haina baraka

(viii) Huwa na mantiki inayokinzana. Mfano
Kawia ufike
Adui mpende

(ix) Hutumia tamathali za usemi. Mfano
Tashbihi- Ufalme kama mvua hupiga na kupita
Kinaya – Bara Hindi ndiko kwenye nguo na wendao uchi wapo
Dhihaka - Mke ni nguo mgomba kupalilia
Tashihisi - Udugu wa nazi kukutania chunguni
Chuku - Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi
Balagha - Umekuwa nanasi kuchumia mibani?
Jazanda - Mimi nyumba ya udongo sihimili vishindo

(x) Hutumika kufunzia (sarufi au fasihi)

(i) Ngeli za nomino
Penye wazee hapaharibiki neno
Kisichofanana na mwenyewe ni cha kuibа

(ii) Msamiati wa viumbe
Fuata nyuki ule asali
Ng'ombe na mbuzi ni wamoja, mtu kando ni kondoo

(iii) Viungo vya mwili
Sikio la kufa halisikii dawa

(iv) Nyakati
Ukitaka kula nguruwe, chagua aliyenona
Ya kale hayanuki

(v) Kinyume
Kawia ufike n.k

Kila hoja ni:
Kutaja sifa Alama 1
Kutaja methali na maelezo Alama 1
Zozote 5 x 2= 10

**UMUHIMU WA HADITHI:**

- Hufurahisha
- Huliwaza
- Huadilisha
- Huelimisha
- Huonya
- Huimarisha umoja
- Huipa jamii mweleke

**SWALI 5**

a) Maghani ni nini? (alama 2)
b) Eleza fani zifuatazo za maghani (alama 8)
  i) Vivugo
  ii) Tondozi
  iii) Pembezi
  iv) Rara
c) Eleza maana ya neno ULUMBI (alama 1)
d) Bainisha sifa za mlumbi (alama 6)
e) Eleza umuhimu wa ulumbi (alama 3)

# jibu

a) Maghani ni utungo wa kishairi ambao hutongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji..

b) i)**Vivugo** ni ushairi wa kujisifia unatungwa papo hapo na fanani mwanaume.
ii) **Tondozi** – utungo wa kutukuza watu, wanyama, vitu kama magari, miti, milima n.k.
iii) **Pembezi** – ni aina ya tondozi ambayo imekusudiwa kusifia watu na aina Fulani katika jamii kutokana na matendo yao au mchango wao katika jamii.
iv)**Rara** – Ufungo wa kishairi wenye ubunifu mkubwa unaokusudiwa kusisimua hadhira. ***(Hoja 4 x 2 = 8)***

c) **Maana ya uhumbi**
- Uhodari wa kuzungumza au kuiga mazungumzo kwa usanii na uhodari mkubwa *Alama 1*

d) **Sifa za mlumbi**
- Mwenye ujuzi wa utamaduni, desturi, mila na sheria za jamii (mzingiro) ujuzi mkubwa wa maisha
- Ufundi wa kutumia lugha, semi, mafumbo nk
- Uwezo wa kutumia mbinu mbalimbali za kuwasiliana mfano, nyimbo, ushairi n.k.
- Umahiri wa kughani, kusema kwa mfululizo na mwendo wa kasi
- Kutumia sauti inayosikika bila shida
- Ufundi wa kutumia kunga za maswali. ***(6 x 16)***

e) Umuhimu wa ulumbi
-Kipimo cha kimsingi cha mtu kuteuliwa kama kiongozi
- Njia maalumu inayotumiwa na jamii kupitisha ujumbe muhimu
- Njia ya kudumisha utamaduni n thamani za kitamaduni kwa kuzionea fahari
- Ni kitambulisho muhimu kwa jamii na wanajamii.

## SWALI 6

1. (a) (i) **Taja** mbinu zozote tatu za kuhifadhi fasihi simulizi (alama 3)
(ii) Taja aina zozote tatu za vitendawili (alama 3)
(iii) Bainisha matumizi ya lugha katika vitendawili (alama 3)

(b) (i) Ngomezi ni nini? (alama 1)
(ii) Eleza ujumbe uliowasilishwa na ngomezi katika fasihi simulizi. (alama 3)
(iii) Fafanua sifa zozote nne za ngomezi. (alama 4)
(iv) Taja mifano mitatu ya ngomezi ya kisasa. (alama 3)

**JIBU**

6. (a) Mbinu za kuhifadhi fasihi simulizi
(i) Katika akili ya binadamu
(ii) Maumbile na mazingira – k.m fisi kuchechemea, kinyonga kutembea polepole
(iii) Katika vifaa meme k.m video
(iv) Katika michoro 3 x 1= 3

(ii) aina tatu za vitendawili
(i) Sahili – vitendwa vinavyoundwa kwa maneno machache
(ii) Tate – huwa ni fumbo linalohitaji kuchemsha bongo ili kung'amua jawabu
(iii) Simulizi – husimulia hadithi kama msingi wa kitendawili.
(iv) Tanakali – huundwa kwa maneno yanayoiga sauti inayotolewa na kitendo k.m chururu si ndo!ndo!ndo!
(v) Mkufu – huwa sehemu zinazohusiana na kuchangizana kimaana na vina urefu Fulani
3 x 1 = 3

(iii) Matumizi ya lugha katika Vitendawili
(i) Taswira – km kuku wangu katagia mwibani. (nanasi)
(ii) Sitiara – Nyumba yangu haina mlango (yai)
(iii) Kejeli – Uzi mwembamba umefunga dume kubwa (Usingizi)
(iv) Tashihisi – popote niendapo amenifuata (kivuli) 3 x 1 = 3

(b)
(i) Ngomezi Ni fasihi ya ngoma

1 x 1 = 1

(ii) Ujumbe uliowasilishwa na ngomezi

(i) Kuzaliwa kwa mtoto
(ii) Ndoa
(iii) Kifo
(iv) Uwindaji
(v) Vita vya kikabila
(vi) Majilio ya mvua
(vii) Kuwaita kwa mchezo wa mleleka
(viii) Kuwaita watu kwa jambo la dharura 3 x 1 = 3

(iii) Sifa za ngomezi

(i) Si rahisi kupata ujumbe wa ngomezi kama wewe si mshiriki wa utamaduni husika
(ii) Ngoma ni muhimu kupitishia ujumbe
(iii) Wanajamii tu ndio wanaoweza kufasiri mdundo wa ngoma na kufasiri maana
(iv) Ujumbe wa dharura huwasilishwa kwa njia ambayo si ghali ikilinganishwa na njia nyingine
(v) Mapigo yanayotolewa kwa maana maalumu huambatana na ngoma inayoeleweka kwa ujumbe mahsusi
(vi) Huongozwa na watu teule katika jamii. 4 x 1 = 4

(iv) Mifano mitatu ya ngomezi uya kisasa

(i) Milio ya ambulensi na magari ya polisi na mazimamoto
(ii) Ving'ora
(iii) Kengele (shuleni, mahakamani, kanisani)
(iv) Toni za kengele za rununu

**SWALI 7**

a) Tofautisha baina ya

(i) Hurafa na Hekaya. (alama 4)
(ii) Hadithi za mazimwi na hadithi za mtanziko. (alama 4)
(iii) Usuli na visasili. (alama 4)

He! He! He! Weee!
Unayeogopa kutahiriwa
Nani atatahiri badala yako
Eh, eh…. Ni babu yako
Eh, Eee!.... kisu kikali mno!
Lakini nitavumilia.

b) (i) Wimbo huu huitwaje? (alama 1)
(ii) Nini dhamira ya wimbo huu? (alama 2)
(iii) Taja sifa zozote tano za utanzu wa nyimbo kwa jumla. (alama 5)

**<u>JIBU</u>**

6. a) Huwafa na Hekaya

i) Hurafa Inahusisha wanyama pekee na huwapa uwezo wa binadamu.
Hekaya Huweza kuchanganya wahusika wanyama na bindamu.
(2 x 2)

ii) Mazimwi Mazimwi huchukua nafasi kubwa hasa kuonyesha ulafi, tama na uovu.
Mtanziko Mhusika mkuu hujikuta katika hali ngumu ya uamuzi kati ya hali mbili au zaidi.
(2 x 2)

iii) Usali Hueleza asili chanzo ayuasili ya watu fulani na maendeleo yake au asili ya mambo kama vile kifo.
Visaasili Asili ya tabia Fulani hasa za wanyama. Huelezea sababu ya mambo kutokea kama yalivyo.
(2 x 2)

b) (i) Nyiso (alama 1)
(ii) Kumpa nguvu/himiza anayeenda jandoni. Asiogope.
(alama 2)
(iii) Sifa za nyimbo.

- Huongozwa na mtu mmoja au wawili kati ya wengine.
- Huweza kuandamana na ala na mfano; zeze, kayamba, ngoma n.k.
- Hufunganishwa na muktadha Fulani mfano, harusi, kifo, jandoni n.k.
- Kila ujumbe huwa na ujumbe maalum.
- Hubadilika kutengemea majira / wakati.
- Ujumbe waweza kuwa wazi au fiche.

Zozote 5 x 1 = 5

**SWALI 8**

6. (a) (i) **Eleza** maana ya misimu (alama 1

(ii) Kuchipuka kwa misimu kunategemea mambo mengi. **Taja** matano miongoni mwa haya. (alama 5)

(iii) **Eleza** muhimu wa misimu katika jamii (alama 4)

(b) (i) Nini maana ya ngomezi? (alama 2)

(ii) Ngomezi ina umuhimu gani? (alama 5)

(iii) **Taja** udhaifu wa ngomezi katika kuwasilisha ujumbe katika jamii (alama 3)

**<u>JIBU</u>**

5. (i) Maana ya misimu

- ni usemi ambao huzuka katika lugha na kutoweka baada ya muda Fulani.

1 x 1 = 1

(ii) Mambo ambayo ni msingi wa kuchipuka kwa misimu

(i) Rika na umri wa watumizi k.m vijana, wazee
(ii) Mazingira – sokoni, bandarini, shuleni
(iii) Mada husika – mavazi, mtu
(iv) Jinsia inayohusika
(v) Sababu za kutumia – kuficha siri n.k

(vi) Tabia za watumizi – walimu, wachokozi n.k

Zozote 5 x 1 = 5

(ii) Umuhimu wa Misimu
(i) kuhifadhi siri
(ii) kuonyesha ubabe fulani
(iii) Kujitambulisha na kundi fulani – la vijana, ngoma n.k
(iv) Urahisi wa kusema mambo bila usumbufu wa kufuata kanuni
(v) Kupamba lugha
(vi) Kuongeza maneno mapya katika lugha

Zote 4 x 1 = 4

B) (i) Maana ya ngomezi

- fasihi ya ngoma/ile hali ya kutumia mapigo ya ngoma kuwasilisha ujumbe Fulani bila wahusika kuukariri au kuutamka.

1 x 2 =

(ii) Umuhimu
(i) Si ghali kuwasilisha ujumbe
(ii) Maadui hawawezi kujua siri zenu
(iii) Kuhifadhi historia
(iv) Kuendeleza utamaduni
(v) Kukuza umoja

5 x 1 = 5

(iii) Udhaifu
(i) Si kila mtu anaweza kutafsiri ujumbe unaokusudiwa
(ii) Husikika na idadi ndogo tu ya watu.
(iii) Mapigo yanaweza kuhitilafiana

3 x 1 = 3

**<u>SWALI 9</u>**

(a) (i) **Fafanua** maana ya methali (alama 2)

(ii) **Fafanua** sifa tano za methali (alama 5)
(iii) **Eleza** majukumu matano ya methali (alama 5)
(b) (i) **Eleza** jinsi fasihi simulizi inavyohifadhiwa siku hizi (alama 4)
(ii) **Taja njia nne** za kukusanya fasihi simulizi (alama 4)

## JIBU

(a) (i) Methali: Ni semi fupi za kimapokeo zenye maana mzito na huwa zimejaa busara au hekima (alama 2)

(ii) Sifa za methali
- Zinatumia tamathali mbalimbali
- Zinatumia lugha za kishairi
- Huwa na maana ya nje / juu naya ndani
- Zingine ni ndefu na zingine ni fupi
- Methali zimegawika mara mbili (wazo na jibu)
- Baadhi hutumia msamiati wa wanyama
- Hujikita katika mazingira ya jamii husika
- Kuna methali zinazopingana
- Kuna methali zenye maana sawa.

(iii) Majukumu ya methali
- hufunza maadili katika jamii
- kukashifu, kukosoa na kusuta matendo mabaya
- kuonya na kutahadharisha
- kufariji, kuliwaza na kupongeza
- kuonyesha mahusiano mema yanayotarajiwa miongoni mwa wanajamii
- kupamba lugha / kukuza lugha/kutukuza usanii

zozote 5 x 1 = 5

* lazima mwanafunzi aeleze

(b) (i) uhifadhi wa fasihi simulizi
- maandishi
- kaanda za sauti
- video / pataninga, filamu
- tarakilishi
- mafanani zozote 4 x 1

(ii) njia za kukusanya
- hojaji
- mahojiano
- kushiriki ( kuwa mmoja wa wasilishaji kwa muda)
- kurekodi kutumia vifaa vya kisasa
- makavazi

**SWALI 10**

a) Taja majukumu manne ya Fasihi Simulizi. (alama 4)
b) (i) Mawaidha ni nini? (alama 1)
(ii) Fafanua sifa tatu za mawaidha. (alama 3)
c) Eleza maana na umuhimu wa aina hizi za nyimbo.
(i) Nyiso (alama 2)
(ii) Mbolezi (alama 2)
(iii) Vave (wawe) (alama 2)
d) Taja vijipera vitatu vya maigizo. (alama 3)
e) Fafanua sifa tatu za methali. (alama 3)

## JIBU

Majukumu ya fasihi simulizi.

i) Huburudisha
ii) Huelimisha
iii) Hupa jamii mwelekeo
iv) Huhifadhi historian na utamaduni
v) Huendeleza stadi za lugha / Hukuza sanaa.
vi) Hufundisha
vii) Hukuza ushirikiano.
viii) Ni pato ( zo zote 4x1=4)
b) i) Mawaidha
- Utoaji wa ushauri, maonyo na wosia wenye lengo la kuhimiza mwelekeo na tabia zinazokubaliwa katika jamii.
( 1 x1 = 1)
ii) Sifa za mawaidha
i) Huwa na mawazo mazito kuhusu maisha.
ii) Hutumia lugha iliyojaa misemo, methali na tamathali za sauti.
iii) Hutumia lugha ya kuvutia na ya kubembeleza.
iv) Huhitaji ustadi wa ulumbi/ hutolewa na mtu mmoja.
v) Ujumbe ni wa moja kwa moja/ mfululizo.
vi) Mambo muhimu yenye mafunzo huibuka.
vii) Hulenga maudhui mbalimbali k.m unyago.
viii) Mtambaji anaweza kuwa kijana au mzee bora awe na ujuzi wa jambo hilo.(zo zote 3 x1=3)
c) i) Nyiso ni nyimbo zinazoimbwa wakati wa kupasha tohara.Ni muhimu kuwapa moyo wanaotahiriwa / kuwahamasisha n.k (alama 2)
ii) Mbolezi ni nyimbo zinazoimbwa wakati wa huzuni na majonzi hasa kuomboleza. Ni muhimu kwa kuwafariji waliofikiwa na maafa/ majonzi /msiba. (alama 2)
i) Vave/ wawe ni nyimbo zinazoimbwa na wakulima wakiwa shambani.
Ni muhimu kwa kuwatia nguvu ya kufanya kazi. (alama 2)
d) Vipera vya maigizo.
i) Michezo
ii) Vichekesho
ii) Ngojera
iii) Majigambo
iv) Utambaji
v) Mazingira ( zo zote 3x1 = 3)
e) Sifa za methali)
i) Huweza kutumiwa katika miktadha mbalimbali.
ii) Huwa na maana fasiri mbalimbali (maana ya ndani na maana ya wazi)
iii) Methali hutumia mbinu nyingi kupitisha ujumbe.
Methali nyingi huwa na sehemu mbili. ( zo zote 3 x 1 =

**SWALI 12**

(a) Tofautisha baina ya ulumbi na soga (Alama 4)
(b) Fafanua sifa za ulumbi (Alama 7)
(c) Taja baadhi ya Miviga maarufu katika jamii za Afrika (Alama 3)
(d) Eleza umuhimu wa Miviga katika jamii (Alama 6)

**<u>JIBU</u>**

**2. FASIHI SIMULIZI**

(a) Ulumbi – uhodari wa kuzungumza au kuiga mazungumzo kwa usanii na uhodari mkubwa.
Soga – Utanzu mdogo wa hadithi za fasihi simulizi unaotumiwa kwa ajili ya kuchekesha, kukejeli au kuumbua / kufanyia dhihaka. **alama 2 x 2 = 4**

(b) Sifa za Ulumbi
(i) Ujuzi wa kina wa utamaduni / desturi au mila.
(ii) Tajriba ya maisha – maarifa ya maisha.
(iii) Ufundi wa kutumia lugha,Semi ,mafumbo,methali n.k
(iv) Uwezo wa kutumia mbinu mbalimbali za kuwasiliana k.m Sauti, ishara, milio, vyombo n.k
(v) Umahiri wa kughani – kusema kwa mfululizo na kasi.
(vi) Uwezo wa kutumia kunga za maswali ya balagha.
(vii) Mavazi/mapambo na zana maalum za kuvutia hadhira ngozi, fimbo n.k
(viii) Sauti inayosikika bila shida. **Zozote 7 x 1 = 7**

**C. Miviga Maarufu**

(i) Sherehe za kuzaliwa
(ii) Sherehe za tohara
(iii) Sherehe za ndoa
(iv) Shughuli za mazishi
(v) Sherehe za kutambika
(vi) Sherehe za jando na unyago
(vii) Sherehe za kupatanisha wanajamii /jamii **Zozote 3 x 1 = 3**

**D. Umuhimu**
(i) Kufundisha wanajamii- mambo muhimu
(ii) Msingi wa kusisitiza umuhimu wa kuonyesha shukrani
(iii) Msingi muhimu wa kuwendeleze jadi na desturi ya jamii inayohusika
(iv) Husaidia kuikuza imani ya mwanajamii kwenye jamii yake/Aweze kuionea fahari.
(v) Msingi wa kuiendeleza elimu na utamaduni wa jamii husika
(vi) Kielelezo kizuri cha jinsi jamii yaweza kukuza umoja utangamano na ushirikiano kati ya wanajamii.
(vii) Kusaidia wanajamii wakati wa tanzia / huzuni – vifo,mazishi. **Zozote 6 x 1 = 6**

**SWALI 13**
6. a) Eleza maana ya tanzu zifuatazo za Fasihi Simulizi ( alama 4)
(i) Vitanza ndimi
(ii) Vitendawili
(iii) Ngano
(iv) Nyimbo
b) Taja sifa mbili mbili za kila mojawapo wa vipera vya fasihi simulizi vilivyotajwa kati (alama 8)
c) Eleza umuhimu wa vitanza ndimi. (alama 4)
d) Fafanua uamilifu wa vitendawili katika jamii. (alama 4
**JIBU**

**FASIHI SIMULIZI**
6. A i) **Vitanza ndimi**
-Ni vifungu vya maneno ambayo hutokeza maneno yanayokaribiana ki maana na jinsi yanavyotamkika.
ii) **Vitendawili.** Ni aina za tungo ambazo ni fupi na zinatoa maelezo yanayoishia kwenye swali

iii) **Ngano** -Ni hadithi za … paukwa pakawa zinaishia…. Na wakaishi raha mustarehe.
iv)

**v) Nyimbo**
-Ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Zozote 4 x 1 = 4
B. i) **Sifa za vitanza ndimi**
-Huwa na maneno yanayoleta utata katika utamkaji
-Maneno yanayotamkika hukaribiana sana kimatamshi.
-Ulimi ndio hutatizika kutokana na dhima yake.
-Lengo la vitanza ndimi ni kuburudisha.

**ii) Sifa za vitendawili.**
-Huwa na kitangulizi / kiigizo
-Baadhi ya vitendawili ni kama mafumbo
-Huwa na maumbo mbalimbali mafupi na marefu.
-Baadhi ya vitendawili hutumia maneno yenye ukinzani.
-Kuna vitendawili vya sauti pekee.

-Vitendawili vya kusisitiza maneno.

**iii) Sifa za ngano**

-Hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine
-Maneno au vifungu vingi hurudiwarudia katika uwasilishaji wake.
-Nyimbo hujitokeza sana katika ngano nyingi aidha mtambaji mwenyewe au mmoja wa wahusika ndiye huimba
-Mifano mingi ya wahusika huwa wanyama, ndege au mazimwi ambao huwa na uhusiano na binadamu.
-Mtambaji mara nyingi hupenda kuiga sauti zinazojitokeza katika hadithi au ngano.
-Ngano nyingi huwa na mafunzo fulani katika jamii hasa maadili ya jamii.
-Hadithi huwa na mianzo maalumu mfano. "Hapo zamani za kale" "hadithi hadithi " n.k. pia huwa na miishio maalum " na wakaishi raha mstarehe"
-Ngano mara nyingi mtambaji hushirikisha hadhira yake kwa kuwauliza maswali.
-Baadhi ya ngano huwa na taharuki ya hali ya juu sana.
-Wahusika mara nyingi huwa na tabia na sifa ambazo hazibadiliki kutoka mwanzo wa hadithi hadi mwisho.
-Masimulizi ya ngano nyingi huwa na chuku
-Msimulizi daima hujulisha hadhira yake mwisho wa ngano au hadithi yake.

**Sifa za nyimbo**

-Watu huimba katika hafla mbalimbali au mahali popote penye shughuli.
-Nyimbo nyingi huwa na ujumbe maalum ambao hujitokeza kwa njia za mafumbo au lugha fiche
-Aina mbalimabli za nyimbo huimbwa kwa njia au mitindo tofauti kulingana na ujumbe na mapambo husika.
-Nyimbo huporomoshwa kwa kutumia viambato kama, vigelegele, ngoma, makofi. milusi, firimbi na hata kengele.
-Nyimbo hupumbaza,hufurahisha na kuliwaza kwa njia nyingi.
-Kila wimbo una wakati maalum wa kuimbwa, mahali na hata waimbaji wake.
-Kikundi cha watu chaweza kuimba au mtu mmoja kutegemea azima ya wimbo na muundo wake.

**Umuhimu wa vitanza ndimi**

1.c) -Huboresha matamshi ya maneno
- Hufurahisha na kuchangamsha
- Hutofautisha maana za maneno
- Huleta dhana ya kuwaza haraka.

**Uamilifu wa vitendawili.**

d) -Ni burudani kwa washiriki k.m vijana kutega na kutegua.
- Huwafanya watu wakomaze akili zao kwa njia nyingi (chemsha bongo)
- Hufundisha kuhusu utamaduni, maadili na kazi

-Huwapa watu motisha na moyo wa ushujaa wa kujivunia mifumo ya jamii zetu.
-Hukuza ushirikiano k.m. uhusiano mwema katika jamii.
-Hukuza lugha
-Vitendawili hubadilika na wakati na mazingira
-Hutuwezesha kuelewa yale yote yaliyomo katika mazingira yetu.
-Hujenga motisha ya kushinda masaibu ya maisha, kuwa na wepesi wa kufikiria, kuamua na kutoa jawabu mwafaka la tatizo.
-Huwawezesha watu wawe na stadi ya kukumbuka mazuri na mabaya ya jamii zao.

**SWALI 14**

6 a) Maghani ni nini? (alama 2)
b) Eleza fani zifuatazo za maghani
i) Vivugo
ii) Tondozi
iii) Pembezi

iv) Rara (alama 8)
b) Eleza maana ya neno **ULUMBI** (alama 2)
c) Bainisha sifa tisa (a) za mlumbi (alama 8)

# JIBU

(a) Maghani ni utungo wa kishairi ambao hutongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji.
(b) (i) Vivugo ni ushairi wa kujisifia unatungwa papo kwa hapo aghalabu na janani mwanaume.

(ii) Tondozi – utungo wa kutukuza watu, wanyama vitu kama magari, miti, ng'ombe, milima n.k.

(iii) Pembezi – ni aina ya tondozi ambayo imekusudiwa kusifia watu wa aina Fulani katika jamii kutokana na matendo yao au mchango wao katika jamii.

(iv) Rara: Ni utungo wa kishairi wenye ubunifu mkubwa unaokusudiwa kusisimua.
(Hoja 4 x 2 = 8)

(c) Uhodari wa kuzungumza au kuiga mazungumzo kwausanii na uhodari mkubwa
(alama 2)
(d) – Ujuzi wa kina wa utamaduni, desturi, mila na sheria za jamii
- Mzingiro mpana wa maisha
- Ufundi wa kutumia lugha, semi, mafumbo n.k.
- Uwezo wa kutumia mbinu mbali mbali za kuwasiliana mfano, nyimbo, ushairi n.k.
- Umahiri wa kughani, kusema kwa mfululizo na mwendo wa kasi.
- Kutumia sauti inayosikika bila shida.
- Ufundi wa kutumia kunga za maswali

**SWALI 15**

1. a) Fasihi simulizi ina makundi manne makuu, yataje . al 4

b) Kwa kila kikundi ulichotaja katika swali la 1 (a) , toa mifano miwili ya vipera vya kila kikundi na utoe maelezo mafupi ya vipera hivyo al 8

c) Nyimbo huwa na jukumu gani katika usimulizi al 2
d) Fasihi simulizi ina sifa ya kuhifadhiwa akilini . Eleza udhaifu wa uhifadhi wa akilini.
Al 6

1. **SWALI 16**

a) Taja mbinu zozote tatu zinazotumiwa kuhifadhi fasihi simulizi huku ukitolea mifano
(alama 6)
b) Eleza umuhimu wa kuhifadhi fasihi simulizi (alama 6)
Semi ni utanzu wa fasihi simulizi ambao ni mfupi na uundwao kwa maneno machache au sentensi kadha.Taja na ujadili vipengele vyovyote vinne vinavyojumuishwa na kundi hili 6.
a)
i) Huhifadhiwa na binadamu katika akili yake k.m ngano za usuli na visasili hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
ii) Maumbile na mazingira pia huhifadhi fasihi K.m Fisi daima huchechemea, kinyonga naye hutembea pole pole.
iii) fasihi nyingine huhifadhiwa katika vifaa meme k.m nyimbo magizo na hadithi nyingine huwekwa katika kanda za sauti, video, sidi n.k
iv) Kazi ya binadamu kama vile michoro huhifadhi fasihi – michoro iliyochorwa k.v kabila Fulani likiwinda au likisherehekea huhifadhi matokeo maalum.

**Hoja za kwanza 3 x 2 =6**
**kutaja mbinu alama 1**
**mf – alama 1**

b) Fasihi huhifadhiwa kwa kizazi kijacho ili:-
- kukielimisha mf hekaya
- kukielekeza na kukishauri – methali, ngano, misemo
- Kukionya na kukihatadharisha –methali
- kukiburudisha na kukifurahisha – nyimbo, maigizo n.k
- kukuza uwezo wake wa kufikiri- vitanza ndimi, chemsha bongo, vitendawili n.k

- ❖ Kukifahamisha zaidi kuhusu mazingira na maumbile fulani n.k
- ❖ Kukieleza asili yake (historia) – Visasili, ngono ya usuli.

**kutaja kizazi kijacho alama 1**
**sababu 5x1 jumla (6)**

c)

i) Misimu – semi za muda, pengine kwa rika, kundi mahali na tabaka Fulani
ii) Mafumbo/ chemsha bongo – kauli zenye maana iliyafichwa kwa madhumuni ya kumfikirisha msikilizaji.
iii) Misemo / nahau – maneno ya kawaida ambayo yakiunganishwa na mengine huleta maana isiyo ya kawaida ama isiyoeleweka kwa urahisi
iv) Methali – ni kifungu cha maneno yanayotumiwa pamoja kwa ufundi mkubwa kwa njia ya kufumbwa.
v) Vitendawili – semi za kimafumbo ambayo humpasa anayeulizwa kufumbua.
vi) Kitanza ndimi- ni kihunzi cha maneno; maneno yanayolingana na kushabiana kisilabi huletwa pamoja na kuunda kihunzi cha maneno chenye maana mara nyingi silabi tatanishi huhusishwa.
vii) Lakabu – majina ya kupanga
viii) Shirikina – ni imani au itikadi au desturi zilizoaminiwa

**SWALI 17**

7. a) Tofautisha kati ya methali na semi. ( alama 2

b) Toa mifano miwili miwili ya methali zinazozingatia tamathali zifuatazo;
i) Balagha (alama
ii) Takriri ( alama 2
iii) Ukinzano (alama 2

c) (i) Fafanua vijipera vifuatavyo vya mazungumzo.
1) Utani ( alama 2 )
2) Soga ( alama 2
3) Ulumbi ( alama 2 )
ii) Taja sifa na umuhimu wa soga. ( alama 6 )

<u>**MAJIBU**</u>

**FASIHI SIMULIZI.**

**7. a) i)** Methali ina ujumbe kamili na huwa na avipande viwili.
**ii)** Msemo ni uesmi mfupi unaoficha maana

**b) Balagha**

- Pilipili usizozila zakuwashiani?
- Mla ni mlaleo, mla jana kala nini?

**Takriri**

- Mtoto wa nyoka ni nyoka
- Haraka haraka haina baraka.
- Asiyejua maana haambiwi maana n.k.

**Ukinzano**

- Kupanda mchongoma, kushuka ndio ngoma
- kukopa harusi, kulipa matanga
- kizuri chajiuza, kibaya chajitembeza n.k

**c) i) utani;** Ni kumfanyia mtu mzaha / sitihizai/ dhihaka
**Soga:** Mazungumzo ya kupitisha wakati au porojo
**Ulumbi:** Usungumzi kwa ufasaha, ufundi au ubingwa.

**11. Sifa za soga.**

- Huongezwa chumvi.
- Wahusika hubuniwa au hupewa majina.
- Yana utani

- Huandamana na vichekesho
- Lugha ya kuvutia
- Hadithi fupi fupi zisizo za ukweli. Zozote 6x1=6

**SWALI 18**

6. a) Eleza kikamilifu sifa zozote tano za mtambaji katika fasihi simulizi (alama 10)

b) Fasihi simulizi aghalabu hutambulika kutokana na sifa zake kuu. Jadili.(alama 10)

7. a) Ngomezi ni nini? (alama 2)

b) Eleza umuhimu wa ngomezi katika jamii. (alama 4)

c) Methali zina umuhimu gani katika jamii? (alama 10)

d) Eleza jukumu la fomula za ufunguzi katika hadithi.(alama 4)

<u>**MAJIBU**</u>

**6. (a)Eleza kikamilifu sifa zozote tano za mtambaji katika fasihi simulizi.*(alama 10***

(i) Uwezo wa kuwasilisha hadithi kwa namna inayochangamsha hadhira.
(ii) Ujuzi wa kuweza kuifahamu hadhira yake.
(iii) Ufahamu mpana wa lugha na utamaduni unaohusika.
(iv) Mtambaji mzuri ni mcheshi.
(v) Uwezo wa ufaraguzi.
(vi) Kuzifahamu tabia za binadamu pamoja na kuelewa mikondo katika jamii.

**(b) Fasihi simulizi aghalabu hutambulika kutokana na sifa kuu. Jadili.** ***(alama 10)***

(i) Mtendaji au fanani
(ii) Hadhira
(iii) Pahali.
(iv) Uhusiano wa ana kwa ana.
(v) Kuambatana na mazingira.
(vi ) Utendaji wa maonyesho
(vii) Ugiligili – mwingiliano.
(viii) Tukio, tendo au jambo ***(Zozote 5 x 2= 10)***

**7. (a) Ngomezi ni nini?** ***(alama 2)***

Ngomezi ni fasihi ya ngoma; ujumbe unawasilishwa kwa njia ya ngoma. ***(alama 2)***

**(b) Eleza umuhimu wa ngomezi katika jamii.** ***(alama 4)***

i. Huuwasilisha ujumbe kwa njia nyepesi.
ii. Hudumisha usiri wa jamii Fulani.
iii. Ni njia mojawapo ya kuudumisha utamaduni wa jamii.
iv. Huhakikisha kuwa wanajamii wanaionea fahari jadi yao. ***(4x1=alama 4)***

**(c ) Methali zina umuhimu gani katika jamii.** ***(Alama 10)***

(i) Kuelimisha na kuelekeza wanajamii kuhusu suala Fulani.
(ii) Kuwasilisha maadili muhimu kwa wanajamii.
(iii) Kuhimiza utendaji ili mtu afaidike.
(iv) Kutoa muhtasari wa funzo – hasa katika ngano.
(v) Kuliwaza au kutuliza-hasa wakati mgumu.
(vi) Kufumbata utamaduni wa jamii.
(vii) Kumfunza binadamu azingatie wajibu wake katika jamii.
(viii) Kukosoa au kukashifu matendo mabaya.
(ix) Huonya na kutahadharisha.
(x) Kuonyesha mahusiano mema miongoni mwa wanajamii.

Novels,Updated KASNEB,ICT,College,High School, Primary softcopy notes 0714497530

**Mwisho**

(xi) Kupamba lugha au maongezi. *(Zozote 10x1= alama 10)*

2 **(d)Eleza jukumu la fumula za ufunguzi katika hadithi.** *(alama 4)*

(i) Kuivuta makini ya hadhira.
(ii) Kutambulisha mtambaji wa hadithi.
(iii) Huashiria na kuonyesha mwanzo wa hadithi.
(iv) Huweka mpaka wazi kati ya ulimwengu halisi na ulimwengu wa hadithi.

## SWALI 19

6. (a) **Taja** mifano minane ya tanzu fupi katika fasihi simulizi. (alama 4)
(b) **Fafanua** sifa zozote tatu za mawaidha katika fasihi simulizi. (alama 3)
(c) **Eleza** umuhimu tatu wa ngomezi. (alama 3)
(d) **Eleza** istilahi hizi za fasihi simulizi. (alama 3)
(i) Maghani
(ii) Mapisi
(iii) Misimu / simo
(e) **Fafanua** sifa zozote tatu ambazo mtambaji wa hadithi anastahili kuwa nazo. (alama 3)
(f) **Taja** methali zozote mbili zilizo na dhana ya tashibiha. (alama 2)
(g) **Eleza** sifa zozote mbili za nyumba zinazotofautisha nyimbo na ushairi simulizi (alama 2)

**<u>JIBU</u>**

(i) Methali
(ii) Misemo
(iii) Nahau
(iv) Vitauza ndimi
(v) Vitendawili
(vi) Misimu / simo
(vii) Lakabu
(viii) Mafumbo. Zozote 8 x ½ = (alama 4 )

(b) Sifa za mawaidha.
(i) Huwa na mawazo mazito kuhusu maisha.
(ii) Hutumia lugha iliyojaa misemo, methali na tamathali za sauti.
(iii) Hutumia lugha ya kuvutia nay a kubembeleza.
(iv) Huhitaji ustadi wa ulumbi.
(v) Hutolewa na mtu mmoja.
(vi) Ujumbe ni wa mfululizo / moja kwa moja.
(vii) Mambo muhimu yenye mafunzo huibuka.
(viii) Hulenga maudhui mbalimbali km. unyago.
(ix) Mtambaji anaweza kuwa kijana au mzee bora awe na ujuzi wa jambo hilo.
Zozote 3 x 1 = 3
(c) Umuhimu wa ngomezi

(i) Hutoa taarifa ya kuwafahamisha watu juu ya jambo fulani.
(ii) Hutahadharisha juu ya hatari.
(iii) Hutoa matangazo rasmi kuhusu jambo lolote katika jamii kv harusi.
(iv) Hudhihirisha ufundi wa kisanaa.
(v) Huwatambulisha watu mashuhuri kv. wafalme, machifu, mashujaa au waganga.
Zozote 3 x 1 = 3.
(d)
(i) Maghani ni ufungo wa kishairi ambao hutongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji / kalima.
1 x 1 = 1
(ii) Mapisi ni maelezo ya historia ambayo hayana ubunifu wowote.
1 x 1= 1
(iii) Misimu ni maneno au semi ambazo huzuka wakati au kipindi fulani miongoni mwa makundi

ya watu. 1 x 1 = 1

(e) Sifa za mtambaji

(i) Uwezo wa kuwasilisha hadithi / ngano kwa namna inavyochangamsha.
(ii) Awe mbunifu.
(iii) Anayeifahamu hadhira – wake / waume / watoto / wazee.
(iv) Ufahamu mpana wa lugha.
(v) Anayefahamu utamaduni wa hadhira.
(vi) Mcheshi - kunasa makini ya hadhira.
(vii) Uwezo wa ufaraguzi na kufahamu mbinu zifaazo za sanaa na maonyesho.
(viii) Ufahamu wa tabia za binadamu – mambo yanayofurahisha / udhi.
(ix) Ufahamu wa mikondo mbalimbali ya
(x)
(i) Ujana ni kama moshi.
(ii) Kawaida ni kama sheria.
(iii) Utajiri ni kama umande.
(iv) Usilolijua ni kama usiku wa giza
(i) Takriri
(ii) Kibwagizo
(iii) Nyimbo huwa na mistari mirefu katika ushairi.

**SWALI 20**

8. a) Taja na ueleze aina zozote tano za Hadithi. (alama 5)
b) Tofautisha kati ya
(i) Mbolezi na Bembezi
(ii) Vitendawili na chemsha bongo. (alama 4)
c) Eleza umuhimu wa vitanza ndimi (alama 3)
d) Taja na ueleze sifa nne ambazo mtambaji anapaswa kuwa nazo. (alama 4)
e) (i) Fafanua maana ya methali. (alama 2)
(ii) Taja methali zinazohusu:
a) Kilimo Kuliwaza.

**JIBU**

8 a) **Taja na ueleze aina zozote tano za Hadithi** ***(alama 5)***

- **Khurafa / kharafa** – Masimulizi ya wahusika wanyama yanayotoa ujumbe au mafundisho km fisi, sungura, simba.
- **Visasili (Ngano za usuli)-** Hadithi zinazoelezea asili, chanzo cha tabia, maumbile fulahi km kwa nini Fisi huchechemea.
- **Mighani / visakale** - Masimulizi kuhusu mashujaa km Luanda magere.
- **Hekaya –** usimulizi wenye ubunifu mkubwa kueleza tukio la kustaajibisha na kuchekesha wahusika huwa binadamu km hekaya na Abunwasi.
- **Miviga** – masimulizi kuhusu sherehe au ibada fulani na kutoka jamii fulani yanayofanyika wakati na mahali maalum. Km kutawazwa kwa viongozi, harusi, jandoni, mazishi n.k .
- **Ngano za mazimwi-** masimulizi yahayohusu majitu ya ajabu yanayoogofya na yenye sifa za ajabu.
- **Ngano za kijanja** – Masimulizi ya wanyama wadogo wanaotumia ujanja kujinasua katika mitego.
- **Ngano zamataziko** – masimulizi ya mhusika kupambana na hali ngumu za kimaisha kuhusu utata wa maamuzi katika hali mbili au zaidi.

**Tofautisha kati ya mbolezi na Bembezi** *(Alama 2)*

b) (i)-**Mbolezi** – nyimbo wakati wa huzuni / majonzi kusifu aliyefariki, matanga, kuliwaza n.k.
-**Bembezi** – nyimbo za kubembeleza au kuwaongoa watoto / walale / wasilie.
***Alama 2)***
(ii) -**Vitendawili** – fani ya semi yenye maana fiche inayotolewa kama swali na

huhitaji kufikiria ili kujibu / kutoa ufumbuzi.
-**Chemsha- bongo** – Mafumbo ya kufikirisha ambapo umbo la nje
huonekana rahisi lakini huhitaji kuwaza kwa makini ili kutoa maana / sahihi. ( Alama 2)

c) **Eleza umuhimu wa vitanzandimi** ***( Alama 3)***
Vitanzandimi – Fungu la maneno linalotamkika sawa au karibu sana katika sentensi.
i - kuboresha matamshi ya maneno
ii - Kufurahisha au kuchangamsha.
iii - Kutofautisha maana ya maneno.
Iv - kuchangamua akili
v - Huelimisha

d) **Sifa za mtambaji wa fasihi simulizi**
i- **Kuchangamsha** – ili kuteka akili za hadhiria.
ii-Kufahamu hadhira- ili ashughulikie mahitaji ya hadhira km watoto,
wazee n.k
iii- **Ufaraguzi** – uwezo wa kuunda upya hadithi upya au kuibadili.
Iv -ufahamu mpana wa utamaduni wa jamii husika.
V -Ucheshi na ukakamavu ili kunasa makini ya hadhira.
Vi- kuelewa tabia ya watu, kunachowakera, kuwavutia, kiwachukiza

c) Ni semi zenye maana ya ndani inayofunza; ina sehemu mbili na hubeba taswira mbalimbali

**Methali zinazohusu.**
**(i) kilimo** **-** Mchagua jembe si mkulima.
**-** Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.
**-** Ukilima pantosha utavuna pankwisha.
**-** Mkulima ni mmoja, walaji wengi.

**(ii) Kuhimiza** - La leo litendwe leo.
- Penye nia pana njia.
- Kuvunjika kwa mwiko si mwisho wa kupika.
- Yalifopita si ndwele tugange yajayo.

**SWALI 21**
1. (a) (i) Ngano ni **nini**? [alama 1]
(ii) **Eleza** tofauti iliyoko kati ya visasili na visakale [alama 4]
(iii) **Fafanua** majukumu yoyote muhimu ya ngano katika jamii. [alama 5]
(b) (i) **Eleza** umuhimu wa vitendawili katika jamii. [Alama 3]
(ii) **Tega** na **utegue** vitendawili vyovyote viwili vilivyo na lugha ya takriri na lugha ya mlio. [alama 2]
(iii) **Taja** sifa zozote tatu za methali. [alama 3]
(iv) **Taja** methali yoyote iliyo na lugha ya balagha kisha ueleze maana yake ya ndani [alama 2]

**<u>JIBU</u>**
**<u>FASIHI SIMULIZI.</u>**
7. a) i)**Ngano** ni hadithi za kimapokeo ambazo hutumia lugha ya mjazo na hutumia wahusika wa aina mbalimbali kama wanyama ,watu au miti. Alama 2
(ii)**Visasili**
-Ni masimulizi juu ya chanzo au asili ya vitu au matukio katika jamii km chanzo cha kifo
Visa-kale
-Ni masimulizi ya juu ya maisha na matendo ya mashujaa katika jamii Alama 2
(iii)**Majukumu ya ngano**.
i) Kuelimisha
ii) Kuburudisha

iii) Kuchemsha bongo/kufikirisha
iv) Kupitisha utamaduni kutoka kwa kizazi hadi kingine
v) Hubainisha maadili kama utu n.k
vi) Kuimarisha umoja na uhusiano mwema.
vii) Hueleza asili ya matukio mbalimbali
viii) Huipa jamii mwelekio na njia ya kufuata
ix) Husaidia jamii kufahamu namna ya kutatua shida zinazozikumba

Zozote 5x1 = 5

(b**) Umuhimu wa vitendawili**

i) Kupitisha utamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine
ii) Kukuza maadili
iii) Kukuza umoja
iv) Kuelimisha
v) Kuburudisha
vi) Kukuza lugha
vii) Kuliwaza
viii) Kuchemsha bongo/kufikirisha
ix) Kueleza juu ya mazingira 3x1= 3

ii) **I) Lugha ya takriri**

Mfano: huku fungu, huku fungu katikati bahari
Jibu – Nazi

(ii**) Lugha ya mlio**

Mfano: parr mpaka maka
Jibu - utelezi

*Asipotega na kutegua hapati alama 2x1 = 2

**(iii) Sifa za methali**

i) Matumizi ya tamathali za usemi k.m takriri tashbihi n.k
ii) Huwa na pande mbili
iii) Huwa na maana ya juu (batini) na ya ndani (fiche)
iv) Zingine hupingana
v) Zingine hutumia majina ya viumbe – watu ,wanyama nk
vi) Zingine zina sifa za ushairi
vii) Zingine hutumia maneno ya vinyume

Zozote 3x1 = 3

(iv) Methali iliyo na lugha ya balagha na maana yake ya ndani
kwa mfano: pilipili usiyoila ya kuwaashiani?
Maana: hapana haja ya kuingilia au kujihusisha naa mambo yasiyokuhusu. (Alama 2)
Methali alama 1
Maana alama 1

*FASIHI SIMULIZI*

7. a) (i) Eleza umuhimu wa nyimbo katika usimulizi.( Alama 2)
(ii) Taja na kueleza tanzu / aina za nyimbo ( Alama 10)

b) **SEMI**

*Tofautisha semi hizi*

i) Nahau na misimu (Alama 2)
ii) Eleza maana ya nahau hizi (Alama 4)
(a) Hawapikiki katika chungu kimoja
(b) Yeye ni jamvi la wageni
(c) Amemwaga mtama
(d) Amechomekwa mizizi
iii)Taja na kufafanua misimu yoyote miwili.

<u>**JIBU**</u> -

7. a) (i) Eleza umuhimu wa nyimbo katika usimulizi. ( Alama 2)

(ii) Taja na kueleza tanzu / aina za nyimbo ( Alama 10)

c) **SEMI** Tofautisha semi hizi

i) Nahau na misimu (Alama 2)

ii) Eleza maana ya nahau hizi (Alama 4)

(e) Hawapikiki katika chungu kimoja

(f) Yeye ni jamvi la wageni

(g) Amemwaga mtama

(h) Amechomekwa mizizi

iii)Taja na kufafanua misimu yoyote miwili.

## SWALI

a) Fafanua fani zifuatazo za fasihi simulizi (alama 6)

i. Ngano za mtanziko

ii. Mazingira

iii. Kifunga nyama

b) Umeombwa kusimulia darasani mughani wa Fumo Liyongo, eleza namna utakavyofanikisha uwasilishaji wako. (alama10)

c) Je, ni vipi jamii ya kisasa inaendeleza Fasihi Simulizi (alama 4)

## JIBU

7.(i) Ngano za mtanziko

Ni hadithi ambapo mhusika anahitajika kufanya uteuzi katgi ya hali mbili ambapo uteuzi huwa ni mgumu kufanywa.

(ii) Mazingara

Ni maagizo ya uganga wa ramli yaani kupigwa ramli au kutazamiwa

(iii) Kifunga nyama

Ni mashairi ambayo ni ya mafumbo ambayo hufumbua kimakusudi ili washairi wengine wayafumbue

(b) (i) kuihusisha hadhira _kupitia kwa ,kuuliza maswali ilikuepuka ukinafu

(ii) kufumia vizianda lugha/ishara _ili kusisitiza ujimbe

(iii) Matumizi ya maleba _ nij kusisitiza ujumbe au kukatia kisa uhai

(iv) Kwa kutumia ufaraguzi _ kwa kubuni kisa upya ili kufurahisha hadhira

(v) Kwa kutumia fomula ufunguzi_ili kuteka nadhari ya hadhira

(vi) Matumizi ya urudiaji/takriri_ili kusisitiza ujumbe/udramatishaji muhimu

(vii) Kwa kutumia uigizaji_ naman lyongo alivyokuwa akitenda vitu Fulani ili kukitia hai kisa

(viii) Kwa kutumia mfuo wa kidrama_kunyamaza kwa muda Fulani ili kusisitiza jambo fulani

(ix) Kwa kutumia nyimbo _ili kuondoa ikinaifu

(x) Atumie lugha inayoeleweka kwa hadhira yake ilikufanikisha ujumbe

(xi) Kwa kutumia sauti ya kuvutia kwa hadhira ili kufurahisha hadhira zaidi

(xii) Kuwa mkakamavu mbele ya hadhira

(xiii) Kwa kutumia toni/kiimbo tofauti tofauti ili kunasa hisia za hadhira.

ZOZOTE 5×2=10

(C)(i) Kupitia kwa tamasha za muziki na drama katika shule nyimbo za kienyeji huimbua

(ii) Kuna mbinu za kisasa za kuhifadhi fasihi simulizi kama maandishi ,sidi na

tarakilishi

(iii) Baadhi ya idhaa za utangazaji huandaa makala ya fasihi simulizi ya baadhi ya jamii zetu

(iv) Sekta ya uhariri inaendelea kifasihi simulizi

(v) Fasihi simulizi ni somo linalofunzwa na kutahiniwa katika shule na vyuo

(VI) Katika sherehe za kitaifa,mawasiliano ya nyimbo na maigizo kutoka tamaduni mbalimbali huwepo

# SEHEMU E: USHAIRI

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

1. Hayawani nondokeya, nondokeya nenda mbali
Melaniwa huna haya, leo haja kukabili
Kimbiya nenda Ulaya, upi ndo wako usuli?
Umbakaji haini.

2. Watoto waulizani, changudoa mekushinda?
Umezua vya uhuni, kuyachafua makinda
Pinga kama si punguani, adilifu mekushinda
Umbakaji haini.

3. Wahanyahanya yayaya, mitaani patupatu
Matendoyo kubwayaya, umewasinya wenetu
Nairobi na Siaya, kote kote lithubutu
Umbakaji haini

4. Jogoo kuparagia, kifaranga ni halali?
Ukimwi wawapatia, huna akili kamili
Nakutungia sheria, takufunga ukubali
Umbakaji haini.

**MASWALI**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama1)
b) Shairi hili ni la bahari gani? Thibitisha jawabu lako. (alama4)
c) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa pili. (alama2)
d) Taja na ueleze tamathali za lugha tatu alizotumia mshairi. (alama3)
e) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama4)
f) Taja matendo yoyote matatu mabaya ya anayesemwa. (alama3)
g) Eleza jinsi mshairi alivyotumia uhuru wake wa utunzi. (alama3)

**MAJIBU**

**USHAIRI**

a) Anwani:
Uhayawani, ubakaji, ukimwi, dhuluma

***Yoyote 1 x 1 = alama 1***

b) Bahari
i) Tarbia – mishororo minne kwa kila ubeti
ii) Ukaraguni – vina vinabadilika badilika kwa kila ubeti
iv) Mathnawi – Lina vipande viwili: ukwapi na utao
v) iv) Msuko – kibwagizo kimefupishwa

***Hoja 4 x 1 = alama 4***

c)Mbakaji anawabaka watoto wadogo ilhali angeweza kuwapata hawara. Pia amepungukiwa na akili na uadilifu. ***2x1 =alama 2***

d) Tamathali za lugha
i) Jazanda – Jogoo kuparangia kifaranga
ii) Tasfida – Changudoa ni Malaya
iii) Stiara – Hayawani, makinda

iv) Maswali balagha – Upi ndo wako usuli?
Changudoa mekushinda?
Jogoo kuparangia kifaranga ni halali?

***Zozote 3 x 1 = alama 3***

e) Lugha nathari

Msanii anasema kuwa si haki kwa mtu mzima kuwadhulumu watoto, na kuwaharibia afya kwa kuwaambukiza ukimwi kwani hiki si kitendo cha akili timamu. Anasema kuwa sheria kali inatungwa ili kutoa adhabu kali kwa mbakaji haini.

***4 x 1 = alama 4***

f) Matendo maovu
   i) Ubakaji
   ii) Kuambukiza watoto ukimwi
   iii) Kuzurura ovyo (kuhanyahanya) mitaani
   iv) Kuwaudhi (kuwasinya) watoto ***Zozote 3 x 1 = 3***

g) Uhuru wa mshairi
   i) Inksari – kufupisha maneno k.m
   mekushinda – wamekushinda
   ii) Tabdila – Kubadili sauti katika silabi ya mwisho k.m
   nondokeya – niondokee
   iii) Kuboronga sarufi – k.m.

Upi ndo wako usuli?
Badala ya
Usuli wako ndiyo upi? ***Hoja 3 x 1 = alama 3***

**Soma mashairi kisha uyajibu maswali.**

**Shairi A**

Baba panga walinoa, makali kutia
Nini kigumu zidia, wataka katia?
Pekeo wajisemea, mori kuzidia
Baba naogopa!

Baba kiiona hiyo, mikunjo pajini
Tabasamu uli nayo, haipo usoni
Inaogofya surayo, umekosewani?
Baba naogopa!

Moyoni wajiwazia, kichwa kutikisa
Jambo gani fikiria, mtima kugusa
Unapanga kipangua, moyo kukuasa
Baba naogopa!

Baba unatufungia, nyumbani mo kweli
Panga linanitishia, lilo na makali
Baba nini yako nia, jibu langu swali
Baba naogopa!

Baba mwili wakucheza, meno kakenua
Mboni nyekundu tuliza, kaka kakazia
Baba sichoki kuliza, niayo nambia
Baba naogopa!

Baba kiwa ni azima, kutaka tuuwa
Tufukuze tu wazima, Mola hurumia
Tungawa hatuna mama, mja saidia
Tuna haki kwishi!

A! Baba kaka kafyeka, umeshamuuwa!
Kakukoseani kaka, huruma nonea
Na mwingine umeshika, hata naye pia?
Baba situuwe!

Masikini ndugu zangu, njoni tukimbie
Shikeni kiganja changu, mbali kimbilie
Mili yenu ole wangu, barafu fanoe
Baba meshauwa!

Baba na wa tatu naye, wanao damuyo
Ona kijito damuye, wapi imaniyo?
Jiwe huruma usiye, katili wa moyo
Baba situuwe!

Baba wanijia pia, nami kumaliza
Wa nini ulituzaa, bila ya kuwaza
Na kifo kuhitimia, kukuza soweza
Baba waniuwa!

**SHAIRI B**

Pindi ilipomjia, Khabari za binti kazaliwa,
Uso ulimsawijika, kwa soni akachanganyikiwa
“Hii ni nukhusi?
Aka, ni nakama!
La, ni neema!
Bali si beluwa?”
Wapi uso aufiche?
Au mchangani auzike?
Izara hii asiipate!
Ya kuzaliwa ‘mke’.
Nitawatolea kisa…...
Nawatangulizia sasa,
Kisa kilichoanza
Kinachoendelea hasa,
Hakijawahi kukoma,
Baharini wala bara,
Kote kimeenea,
Namna wanavyomtesa,
Kiumbe dhalili wamemfanya,
Lini atathaminiwa?
Kisa chenyewe kitendawili,
Mwenye busara atoe taawili,
Ya haya mambo mawili;
Maisha bila ‘mke’ ni awali,
Kisa kingeendelea?
Lulu iliyohifadhiwa ni la pili,
Kisa kingeendelea?

**Maswali**

1. Lipe shairi la A kichwa mwafaka (alama 2)
2. Eleza dhamira ya: (alama 4)
   (i) shairi A.
   (ii) shairi B.
3. Taja arudhi za shairi A. (alama 4)

4. Fafanua ujumbe wa shairi B. (alama 2)
5. Shairi A ni la bahari gani? Toa ithibati. (alama 4)
6. Andika ubeti wa nane wa shairi la A kwa lugha ya nathari. (alama 4)

# .SHAIRI

# a) jibu – shairi

-Baba naogopa
-Baba usituwe
-Baba! ***Chochote 1 x 2 = 2***

**b) i) Mtoto analalamika babake kuwazaa.**
-Anaona aibu
-Anaogopa
ii) – Baba analalama kuzaliwa binti
- Anaona aibu; utamaduni na jamii kumkejeli ***1 x 2 = 2***

**c) – Jumla ya beti 10**
-Kila ubeti una mishororo mine
-Mishororo mitatu ya kwanza ina migao miwili.
-Kibwagizo kimezukwa ***4 x 1 = 4***

**d)** – Mume alalama / alalamika
**-**Mkewe kamzalia binti
**-**Bila wanawake maisha hayatakamilika ***2 x 1 = 2***

**e)** Tarbia- Mishororo minne kila ubeti
Msuko – Mshororo wa mwisho kila ubeti umesukwa
Kutaja 2 x 1 = 2
Maelezo 2 x 1 = 2

***f)*** Ndugu zangu masikini njooni tutoroke ili mnishike mkono wangu kwa sababu miili yenu ni baridi.,mfano wa barafu. Baba ameangamiza; ameua. ***4 x 1 = 4***

## <u>USHAIRI.2</u>

***<u>Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo</u>***

-Mkata ni mkatika, harithi hatoridhiwa
Sina ninalolishika, wala ninalochukuwa
<u>Mlimwengu</u> <u>kanipoka,</u> hata tone la muruwa!
Mrithi nini wanangu?

- Sina ngo'mbe sina mbuzi, <u>sina konde sina buwa</u>
Sina hata makaazi, mupasayo kuyajuwa
Sina mazuri makuzi, jinsi nilivyoachwa
Mrithi nini wanangu?

- Sina kazi sina bazi ila <u>wingi wa shakawa</u>
Sina chembe ya majazi mno nikukamuliwa
Nakwa'cheni upagazi, ngumu kwenu ku'tuwa
Mrithi nini wanangu?

- Sina sikuachi jina, mkata hatasifiwa
Hata nifanye la mana, mno mi kulaumiwa
Poleni wangu sana, sana kwenu cha kutowa
Mrithi nini wanangu?

-Sina leo sina jana, sina kesho kutwaliwa
Sina zizi sina shina, wala tawi kuchipuwa
Sina wanangu mi sina , sana la kuacha kuraduwa
Mrithi nini wanangu?

- Sina utu sina haki, mila yangu meuliwa
Nyuma yangu ili dhiki, na mbele imakaliwa
N'nawana na milik, hadi nitakapofukiwa
Mrithi nini wanangu?

- Sina ila kesho kwenu, wenyewe kulongowa
Muwane kwa nyinyi mbinu, mwende pasi kupumuwa
Leo siyo kesho yenu, kama mutajikamuwa
Mrithi nini wananngu?

i. **Taja** mambo yoyote mawili ambayo mtuzi angewarithisha wanawe. (alama 2)
ii. Eleza sababu ya mtuzi kutoweza kuwarithisha wanawe. (alama 3)
iii. **Andika** ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)
iv. **Dondoa** mifano miwili miwili ya : (alama 2)
a. Inkisari
b. Tabdila
v. **Chambua** shairi hili kwa upande wa :
1. Dhamira (alama 2)
2. Muundo (alama 4)
vi. **Eleza maana** ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumiwa katika shairi. (alama 3)
a. Mlimwengu kanipoka
b. Sina konde sina buwa.
c. Wingi wa shakawa.

**1. <u>MAJIBU USHAIRI</u>**

**(a)** – Makazi mabovu
- Upagazi
- Kutothaminiwa
- Dhiki
- Kufanya kesho ya wengine nzuri (zozote 2 x 1 = 2)

**(b)** - Ni maskini hohehahe / hana kitu
- Aliporwa kila kitu.
- Hana mifugo.
- Hana kazi yoyote.
- Hana sifa / umaarufu.
- Ana makazi mabovu.

(zozote 3 x 1 = 3)

**(c)** - Sina jina nitakawacha kwani maskini hasifiwi
- Hata nikifanya jambo la maana ninalaumiwa tu.
- Poleni sana wanangu kwa kuwa sina la kuwatolea.
- Mtarithi nini wanangu?

(zozote 4 x 1 = 4)

**(d)** (i) Inkisari
– Mana – Maana
– Meuliwa – Imeuliwa
– Nitapofukiwa – Nitakapofukiwa.

(zozote 2 x ½ = 1)

(ii) Tabdila
Muruwa - Murua
Kutowa -Kutoa
Kushipuwa -Kuchipua
Kwongowa - Kuiongoa
Kupumuwa - Kupumua

(zozote 2 x ½ = 1)

**(e)** (i) Dhamira
– Kuwahimiza watu kufanya bidii wakiwa vijana.
– Kulalamika kwamba maskini hana haki / huonewa / hapewi nafasi. (1 x 2 = 2)

(ii) Muundo

– Shairi ni aina ya tarbia / unne.Lina mishororo minne katika kila ubeti.
– Mishororo ya kwanza mitatu imegawika katika sehemu mbili (ukwapi na utao).
– Kila kipande kina mizani nane na kila mshororo una mizani kumi na sita.
– Vina vya kati vinatofautiana kutoka ubeti mmoja hadi mwingine, lakini vina vya mwisho ni sawa katika shairi zima katika mishororo ya kwanza mitatu.
– Shairi hili lina kibwagizo ambacho kimefupishwa.

Mrithi nini wanangu?

– Shairi hili lina beti saba.

(Hoja zozote 4 x 1 = 4)

**(f)** (a) Mlimwenngu kunipoka - Mlimwengu kanipokonya.
(b) Sina konde sina buwa - Sina shamba sina chochote.
(c) Wingi wa shakawa – mashaka mengi.
(3 x 1 = 3)

**USHAIRI 3**

**7. Soma shairi lifuatalo kwa makini halafu ujibu maswali yanayofuata.**

1 Kijana tuza makini, nikwambie usikile
Chakula mahotelini, si kizuri usikile
Ufikapo mlangoni, kizingiti usikile

2. Nenda kaseme nyumbani, kesho asubuhi siji
Nitakwenda makondeni, kawashunge shunge siji
Na hata hapo jioni, kama nitakuja siji

3. Na kama wenda mjini, upatapo nyumba panga
Upahame mizimuni, palozingirwa na panga
Hapana tena amani, kutwa mwapigana panga

4. Na kesho kija shambani, uonapo mti panda
Kwea hadi kileleni, ujifiche kwenye panda
Kaziyo ulinde chini, mimea tuliyopanda

5. Kishuka ola shinani, njugu merundika chungu
Njugu peleka nyumbani, zisije zikawa chungu
Kaanga sufuriani, au pia kwenye chungu

6. Kileta maji jioni, ndoo jitwike na kata
Kata njema ya majani, laini wezayo kata
Kumbuka ya kisimani, huteki ela kwa kata

7. Ninawahi kibandani, nikaliezeke paa
Nipate lindia nyuni, na wanyama kama paa
Kwani kiola angani, naona jua lapaa

8. Kisha takwea mtini, nimeona bivu tunda
Sina usono moyoni, ela tunda kisha tunda
Nimpe wangu mwendeni, jioni nishike tunda

9.Meanza wao uneni, hapo nami ndipo kamba
Leo wenda hawaoni, kama wa bahari kamba
Wajijaza kimiani, wakijitatia kamba

10.Mtoto wachoma yakini, japo liwe moja kaa
Ukikupata takoni, ni shida huwezi kaa
Ela hufaa mekoni, kutoka nswi na kaa

**Maswali.**

a) Bainisha dhamira ya mtunzi wa shairi hili alama2)
b) Eleza maana tatu za neno <u>chungu</u> kama lilivyotumika katika shairi (alama3)
c) Andika ubeti wa nane katika lugha nathari (alama3)
d) Eleza muundo wa shairi hili (alama5)
e) Onyesha vile uhuru wa kishairi ulivyotumiwa na malenga (alama4)
f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi (alama3)
 i) Makondeni
 ii) Jitwike
 iii) Kiola

<u>**MAJIBU**</u>

**MWONGOZO WA USHAIRI**

7.

(a) Kufunza maana mbalimbali za maneno (1x2=1)
(b) Maana za neno 'chungu'
 (i) Tele/ ingi
 (ii) Chachu
 (iii) Kifaa cha kupikia (3x1=3)
(c) Nitapanda juu ya mti, mahali ambapo nimechuna tunda lililoiva kwa sababu siwezi kutulia mpaka nilipate ili nimpe mpenzi wangu ndipo jioni niweze kupapasa titi (alama 3)

(d) (i) - Lina mishororo mitatu – ni tathlitha
– Kila mshororo una vipande viwili
– Vina havifanani
– Lina beti kumi
– Mizani 16 (8, 8) (5x1=5)

(e) (i) Tabdila, mfano – usikile – usikie
(ii) Inkisari, mfano – kaseme – ukaseme
- mi - mimi
- kaziyo - kazi yako
- takwea - nitakwea
(iii) Kuboronga sarufi – Na kesho kija shambani
-Na ukija shambani kesho
(iv) Lahaja - Ola,
- Ona (Zozote 2x2)

Kutaja alama 1 mfano alama 1
(i) Makondeni – mashambani
(ii) Jitwike – weka kichwani/ mgongoni
(iii) Kiola – kiona/ kiangalia/ kitazama (3x1=3)

## D USHAIRI 5

**5.** Linganisha na kutofautisha mashairi ya ARUDHI na MASHAIRI HURU (alama20)

**6.** Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

1. Hisani inanyanyuza,
Mdogo ikamkuza,
Kinda ikamtukuza
Hisani ikamlea.

2. Hisani na ukarimu,
Hadi ni vitu muhimu,
Mfanowe mlizamu,
Hisani kufadhiliwa.

3. Hisani kama Johari,
Haipati mjasiri,
Ni Joho lenye fahari,
Hisani ukitumia

4. Basi sikia watoto,
Hisani ni jambo zito,
Si pesi kama kokoto,
Si kitu cha kubeua.

5. Hisani yaweza kupa,
Utajiri kukukopa,
Ukaweza kunenepa,
Lafidhi njema kutoa,

6. Ihisani haiozi,
Mfano kama mizizi,
Zaidi ya utoshezi,
Unapoitumilia.

7. Hisani ni kama fimbo,
Husotea hata ng'ambo,
Ikawavuta warembo
Hisani bila udhia.

8. Hisani njema huweka,
Ni akibayo ya myaka,
Japo wito kiitika,
Hisani itasalia.

9. Ikupe mema makazi,
Wewe na wako uzazi,
Iwe kama sumlizi,
Na wana wakitumia.

10. Basi dunia si fosi,
Yataka mwendo wa ngisi,
Wawapi kina Msosi,
Nguvu walikitumia.

9. Nanyi ndugu fikirini,
Muikumbuke hisani,
Haiozi ihisani,
Daima huchipukia

12. Hisani yanipa sifa,
Yanongeza maarifa,
Na hata kama nikifa
Wanangu watatumia.

13. Watatumia maisha,
Hisani nilobakisha,
Hadi mwisho wa maisha
Na kuondoka dunia,

14. Najua mtakubali,
Haya bila ya shikeli,
Asiyejua fadhili,
Nyama kasoro mkia.

a) Fafanua arudhi zilizotumiwa kutunga shairi hili (alama4)
b) Kina kinachokaririwa sana katika shairi hili huitwaje? (alama1)
c) Shairi hili huitwaje? (alama1)
d) Ukirejelea shairi hili, fafanua sifa za mashairi ya aina hii (alama4)
e) Ni upi ujumbe wa mshairi? Toa mifano minne (alama4)
f) Taja na ufafanue mifano minne ya mbinu za matumizi ya lugha katika shairi (alama4)

g) i) Linganisha na kutofautisha maneno
'Hisani na Ihisani' (alama1)

h) Taja mstari unaolingana kimaana na
'Japo wito kiitika'

**MAJIBU**

**Ushairi**

5. Mlingano

Mashairi haya huru na ya arudhi hufanana kwa njia kadhaa

(i)Maumbo- Yote hutumia sanaa ya lugha kwa njia ya mkato, tofauti na kazi za nathari kama Riwaya n.k.

(ii) Muundo- Mashairi yote hujigawa katika beti, mishororo, vipande, pia mizani

(iii) Kibwagizo- Si lazima

(iv) Matumizi ya lugha -Hutumia lugha:
- Ya mvuto
- Ya mafumbo
- Ya mkato
- Ya kishairi
- Isitiari
- Tamathali za usemi n.k.

Mbinu zingine kama inkisari, tabdila, mazida na uhuru wa utunzi

(v) Wakifishaji- Yote hutumia alama za kuakifisha kama koma, kiulizi kishangao n.k.

(vi) Maudhui - Mashairi yote huwa na ujumbe muhimu wa mtunzi
- Mambo makuu yanayomhusu binadamu na mazingira yake

(b) **Tofauti**

**Huru:**

- Maumbo hubadilika
- Idadi ya mistari kutoka ubeti hadi mwingine hutofautiana
- Lugha sanifu
- Maudhui hutofautiana
- Hutumia viwakilishi kwa kusudi maalum (5 x 1 = 5)

**Mashairi Jadi**

- Maumbo hayabadiliki
- Muundo – idadi ya (i) vipande (ii) mizani (iii) vina huzingatiwa
- Mshairi huwa na uhuru wa kuiboronga lugha ili kutosheleza vina/ mizani
- Maudhui hutofautiana
- Viwakifishi havitumiwi sana (ila koma, kiulizi, kishangao) 5 @ 1=5

6. (a) Arudhi zilizotumiwa

(i) Vina - havitiririki ila katika mstari wa mwisho k.m. ub 1 -zaub.9 -ni
- za - ni
-za - ni
- a - a

(ii) Mizani - 8
- 8
- 8
- 8

(iii) Kipande kimoja tu kila mshororo

(iv) Hakuna kibwagizo (sabilia)

4 @ 1 = 4

(b) Kina chaitwa - BAHARI alama 1

(c) Utenzi alama 1

(d) **Sifa za tenzi**

– Beti nyingi hata mamia k.m. shairi hili lina beti 14

- Mizani ni 8 (kipande kimoja tu)
- Kina cha mwisho kila ubeti huhifadhiwa (hukaririwa)
- Mashairi hushughulikia maswala mazito au ya kihistoria

(e) **Hisani ina faida nyingi**

Ub. 1 - Yamkuza na kumlea mtu hadi ukubwani
Ub. 5 - Yaweza kukutajirisha
Ub. 8 - Ni akiba inayodumu – ukifa itadumu/ hubakia/ itakumbukwa
Ub. 9 - Hukusaidia kupata makazi mazuri
Ub. 10 - Huongeza maarifa na huifaa aila yetu
Kubali jibu lirejealo shairi

(4 x 1 = 4)

f) Mifano ya tamathali za usemi/ mbinu za matumizi ya lugha

(i) Tashihisi/ uhuishi
Ub 1 - hisani inanyanyua
- yaweza kupa utajiri

(ii) Ub 6, 10 - methali
- Dunia mwendo wa ngisi
- Hisani haiozi

(iii) Ub 3,7 - Tashbihi - Hisani kama johari; hisani ni kama fimbo

(iv) Ub 3 - Jazanda - Hisani ni joho la fahari

(4 x 1 = 4)

(g) Ulinganifu - maana ni moja (½)
Tofauti - mizani
Ub 1 - mizani 3
Ub 6, 9 - mizani 4(kufikia urari wa mizani)
Alama ½

(h)msitari unaolingana na ‘Japo wito kiitika - ub. 12- Hata kama nikifa (1mk)

# USHAIRI 7

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Nina machache mabwana,
Kwa nudhumu nitanena,
Na wala shaka hayana,
Napenda kuyaandika.

Sababu tumezidia,
Kuacha ya asilia,
Kazi ilotimilia,
Ambayo imetukuka.

Iwapo kazi hupati,
Usipotewze wakati,
Rudi shamba kata miti,
Na magugu kuyakata.

Haraka tukaze kamba,
Tukimbilie mashamba,
Tukaipande migomba,

Na mimea ya nafaka.

Ukishajijua wazi,
Kuwa wewe huna kazi,
Yapunguze matembezi,
Kuzurura ni mashaka,.

Haya sahibu mwendani,
Sizurure mitaani,
Litie jembe mpini,
Uwache kuhangaika.

Ni kalamu mfukoni,
Suti na tai shingoni,
Twautaka ukarani,
Mashamba twayaepuka.

Tunapokaa mezani,
Shamba atalima nani,
Kisha tutakula nini,
Inataka kukumbuka.

Ni bure wanaosema,
Kudharau ukulima,
Na hali dunia nzima,
Ukulima wasifika.

Haya tununue mbegu,
Tuyalime magugu,
Tusifikirie sugu,
'mikononi' kutushika.

Ni lazima ujikisi,
Ukizitaka fulusi,
Hakuna kazi rahisi,
Hadi jasho kukutoka.

Shima tena waungwana,
Mambo yapate kufana,
Hasa kwa sisi vijana,
Tupendao kuzuzuka.

Tamati tulime sana,
Tushike mengi mashina,
Kwa nguvu zake Rabana,
Itazidia baraka.

**MASWALI**

a) Tambua bahari ya shairi hili. (alama 2)
b) Eleza sifa zozote nne zinazotofautisha bahari hii na mashairi mengine. (alama 4)
c) Mwandishi ameshughulikiaje 'utoshelezi wa mawazo' katika ubeti
wa 7, 8 na 9? (alama3
d) Fafanua. (alama 2
i) Mleo wa ubeti wa sita.
ii) Mloto wa ubeti wa mwisho.

e) Endeleza ubeti wa 12 wa shairi kwa lugha nathari. (alama 3)
f) Eleza dhamira ya mshairi huyu. (alama 3)
g) Andika maana ya maneno haya kama yalivyotumika. (alama 3)
i) Nudhumu
ii) Sugu
iii) Fulusi

**USHAIRI MAJIBU**

a) Utenzi.

**b) Sifa za utenzi**

i) Mizani zisizodidi 12 katika mshororo
ii) Kipande kimoja tu katika mshororo
iii) Huwa na beti nyingi
iv) Huzungumzia maswala mazito m.f siasa, dini, ndoa.
v) Huwa na kina sawa katika kiitikio ***3 x 1 = 3***

**c) Utoshelezi wa mawazo**

Ubeti wa 7 – Watu huvalia nadhifu kutafuta kazi za ukarani, wakapuuza za mashambani.
8 – Iwapo sote tutataka kazi za ukarani nani atalima / atakuza chakula?
9 – Tusidharau ukulima maana wasifiwa kote duniani***(3 x 1 = 3***

d) i) Tuzike mengi mashina – tupande mimea mingi
Litie jembe mpini – tujiandae kwenda shambani **2 x 1 = 2**

**e) Lugha natharia – ubeti wa 12**

- Ninawahimiza wenzangu mjitahidi ili sisi vijana wajinga tuweze kufanikiwa.

***Alama 3***

**f) Dhamira**

- Tusichague kazi
- Kilimo ni bora / muhimu
- Tusizurure mjini kutafuta kazi ***(3 x 1 = 3)***

**g) Maana ya:**

i) Nudhumu – Shairi
ii) Sugu – Malenge/ enge/ kuchibuka mikononi
iv) Fulusi – Pesa / ngwenje/ mapato

**v) USHAIRI 8**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

**1**

Ameumbwa mwanadamu, kwa lililo zuri umbo
Bali si wote fahamu, waliyo na sawa mambo
Wako waliyo timamu, na wengineyo wa kombo
Na mtu kuwa na tumbo, si kwamba mekamilika

**2**

Kuna walo mafidhuli, lugha yao ni matango
Na kuna wenye kauli, zisokuwa na ushingo
Kuna wake kwa <u>wavuli,</u> vipofu na wenye tongo
Na mtu kuwa na shingo, si kwamba mekamilika

**3**

Kuna walo na fikira, na wenye vibovu vitwa
Kuna walo na subira, husubiri kucha kutwa
Wengine tabiya bora, hino hawanayo <u>katwa</u>
Na mtu kuwa na kitwa, si kwamba mekamilika

**4**

Kukamilika kwa mja, ni mbali na kwa Moliwa
Kwa mja nitakutaja, ili upate kwelewa
Ni kufikiya daraja, ile aliyoumbiwa

Hapo ndipo huambiwa, mja amekamilika

**5**
Aiyelewe duniya, kwa marefu na mapana
Azipite zile ndiya, za miba mitungu sana
Avuke bahari piya, zilo na virefu vina
Hiyo ni yangu maana, ya mja kukamilika
**6**
Akishafikwa na hayo, si kwamba ndiyo akhiri
lazima awe na moyo, wa kuweza kusubiri
Kuyasubiri ambayo, yote yatayomjiri
Kama huyo 'tamkiri, ni mja mekamilika.

7. a) Kwa kuzingatia shairi, fafanua mambo muhimu yanayomfanya mtu kuwa na utu. (alama 5)
b) Andika ubeti wa 5 kwa lugha ya nathari. (alama 4)
c) Eeza muundo wa shairi. (alama 4)
d) Onyesha kwa kutoa mifano, uhuru wa kishairi alioutumia mtunzi.(alama 4)
e) Eleza maana ya maneno haya yalivyotumika katika shairi. (alama 3)
(i) Wavuli
(ii) Katwa
(iii) Akhiri.

**MAJIBU** Zozote 5 x

7. Kutokuwa fidhuli
a) Kuwa na zubira
Tabia bora
Kuwa na fikra nzuri
Kuwa na lugha nzuri/kauli nzuri
Aulewe dunia

Zozote 5 x 1 = 5

b) Mtu aliyekamilika ni yule anayeielewa 1
dunia kinagaubaga ambaye amejifunza mengi 1
na amepata shida za kilimwengu na akazishinda. 1

c) Kila ubeti una mishororo 4
limegawanywa kwa vipande viwili (ukwapi na utao)
vina vinabadilika badilika beti hadi beti
mizani 16 kwa kila mshororo.

4 x 1 = 4

d) Inkisari - Mekamilika, kwelewa n.k.
lahaja - Vitwa, ndiya n.k.
tabdila - Waliyo tabiya
Mazida - Meliwa

½ - Taja 2
½ - Mfano 2
4

e) Wavuli - Wavulana
Katwa – Kamwe/asilani/kabisa
Akhuri - Mwisho/tamati/kikomo

**USHAIRI – S . KUVUNA**
Babu: Jina hili limevuma , mjini shambani pia
Gazetini wanasema, mara nyingi hutokea
Nashindwa pa kutuama , makelele yamejaa
Ukimwi ninauliza , kitu hiki kitu gani?

Bibi: Sihangaike bwanangu, jambo hilo kutuhusu
Dunia ina mizingu, shika yanayotuhusu
Mambo mengi chunguchungu, ni vigumu kudurusu
Ukimwi nimesikia, kila mtu yuataja
Babu: Nikifungua radio, matangazo yazagaa
Kenya nayo hata hio, Tanzania yaongea
Jihadhari na kinoo, Ukimwi ukisambaa"
Ukimwi ninauliza, Kitu hiki kitu gani?
Bibi: Jambo umeshikilia , Ukimwi sijui nini?
Shika njia kimbilia , Uliza wanake nini?
Mashaka yamezidia , Waweweseka ndotoni?
Nyuma tusijiachie , mashaka kujiwekea
Babu: Ni vyema tuutambue, twende kwa wanaojua
Akili watufumbue, tufahamu ya dunia.
Nyuma tusijiachie, mashaka kujiwekea.
Ukimwi ninauliza, kitu hiki kitu gani?
Bwana afya: Sijidanganye mzee, ukimwi hauna dawa.
Na mabingwa waendee, kufanyiza na daawa.
Wataushidwa umee, ukukate kama buwa.
Ni ugonjwa wa hatari , jiepushe na ukimwi
Bibi: Serikali twapongeza , hatua imechukuwa
Wagonjwa kuwachunguza , na viini kufichuwa
Imetoa mwangaza, imepiga nyingi rewa
Ni ugonjwa wa hatari , jiepushe na ukimwi .

Babu: Tamati hapa tuwatia, ujumbe mmeupata .
Kupuuza ni hatia, wajiletea matata.
Uache kupuuzia, dawa kamwe hutapata .
Ni ugonjwa wa hatari , jiepushe na ukimwi.

**Maswali**

a) Fafanua umbo la shairi hili . alama 5
b) Andika ubeti wa tano katika lugha nathari alama 4
c) Fafanua matumizi ya uhuru wa kishairi katika shairi hili . alama 6
d) Serikali inafanya juhudi gani kupambana na janga hili kwa mujibu wa shairi alama 2
e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi
i) Mizingu
ii) Waweweseka
iii) Daawa alama 3

## MAJIBU

### A. SHAIRI

7. (a) – Ni ngonjera
- Lina mishororo 4 katika kila ubeti
- Lina beti 8
- Vipande viwili
- Vina vinabadilikabadilika
- Mizani 16

(Hoja 5 x 1=5)

(b) – watuelimishe tuelewe
- Tusibakie mashakani kwa kutoelewa
- Ama kweli, ukimwi ni nini?

(Hoja 4 x 1=4)

(c) – Kuna upondaji wa sarufi ili kuabikia arudhi za vina kwa mfano mara nyingi hutokea – badala ya hutokea mara nyingi (ubeti wa 1)

- Urefushaji/mazida kuabikia idadi ya mizani katika mishororo kwa mfano: yamezidia – badala ya yamezidi (ubeti wa 4), tusijiachie –badala ya tusijiache (ubeti wa 5)
- Ufupishaji / inkisari kuafikia idadi ya mizani katika mishororo kwa mfano:

Nashindwa - ninashindwa (ubeti 1)
Manake – maana yake (ubeti 4)

(Hoja zozote 3 x 2 = 6)
Kutaja uhuru – alama 1
Kutoa mfano na ufafanunizi – alama 1

(d) Kuwapima wagonjwa

- Kutoa maelezo kuhusu ugonjwa huu
- Kutoa matangazo ya tahadhari (zozote 2 x 1=2)

(e) (i) Mitego, sumbuko
(ii) Unahangaika, unababaika
(iii) Kesi, mashtaka Hoja 3 x 1 = 3)

1. **<u>USHAIRI</u>**

***<u>Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali</u>***

1. Ulimwengu huu wetu, wa zama hizi za sasa,
Ni wa kulinda misitu, ndovu chiriku na kasa,
Pamoja na ardhi yetu, zisipatwe na mikasa,
Ni wajibu wetu sote, kuyalinda mazingira.

2. Wanaonyesha njiya, kutimiza hii nia,
Ni wazungu wa Ulaya, na mataifa ya Asia,
Marekani inaliya, mengi ikikatalia,
Ni wajibu wetu sote, kuyalinda mazingira.

3. Jumuiya ya dunia, mikataba imeweka,
Kujaribu kuzuia, majanga kwetu kufika,
**Kiyoto*** ilianzia, mazimio kupitika,
Ni wajibu wetu sote, kuyalinda mazingira,

4. Mataifa ya viwanda, yatoayo nyingi gesi,
Yasijifanye **makanda**, ya **Kiyoto** kuyaasi,
Yakiguguna ukanda, wa ozoni **ndio basi**,
Ni wajibu wetu sote, kuyalinda mazingira.

5. Tatizo la Afrika, lihusulo mazingira,
Ni misitu kuifyeka, kujiletea hasara,
Udongo kumomonyoka, shamba 'kawa barabara,
Ni wajibu wetu sote, kuyalinda mazingira.

6. Katika hii **kadhia**, ya kuyalinda mapori,
Tunaye **gwiji** sikia, ni Profesa Wangari,
Zawadi kaipokea, alipoenda safari,
Ni wajibu wetu sote, kuyalinda mazingira.

7. Profesa msifika, kwa kazi yake **jamali**,
Oslo yeye kafika, huko Ulaya ya mbali,
Wazungu walimwalika, wakamtuza NOBELI,
Ni wajibu wetu sote, kuyalinda mazingira.

8. Hotuba zikatolewa, kumsifu mwanakwetu,
Maombi akaombewa, ajaliwe barakatu,
Nyimbo nazo kaimbiwa, za ng'ambo na za kikwetu,
Ni wajibu wetu sote, kuyalinda mazingira.

9. Wangari hana utani, wala hatumii fosi,
Mifufu, mizeituni, mipingo na mifenesi,
Asema, 'Nyote njooni, tuipande kasi kasi,
Vijijini na mijini, tusibakize nafasi,
Ni wajibu wetu sote, kuyalinda mazingira.

* ***Kyoto*** *ni mji katika Ujapani ambapo mikataba kuhusu mazingira itiliwa saini.*

(a) **Lipe** kichwa shairi hili (alama 2)
(b) **Eleza** dhamira ya mshairi (alama 2)
(c ) **Eleza** umbo la shairi hili (alama 2)
(d) **Andika** ubeti wa sita kwa lugha ya nathari (alama 4)
(e) Maneno yafuatayo yana maana gani?
(i) Makanda
(ii) Gwiji
(iii) Jamali
(iv) Fosi (alama 4)
(f) Onyesha jinsi uhuru wa mshairi umetumika katika shairi hili (alama 1)

**USHAIRI MAJIBU**

7. (a) kuhifadhi mazingira
- kutunza mazingira
- kulinda mazingira 1 x 2 = 2

(b) kuhamasisha, kushauri, kihimiza, kuelimisha watu wote kulinda mazingira(alama 2)
(c) Mishororo mine (tarbia) isipokuwa ubeti wa tisa
-beti la tisa
-ukaraguni
-lina kibwagizo ( Ni wajibu wetu sote kuyalinda mazingira)
-vipande viwili
-Mizani 8, 8 isipokuwa ubeti wa tano mshororo wa kwanza , ubeti wa sita mshororo wa pili na ubeti wa saba mshororo wa kwanza.
(d) katika shughuli / harakati za kulinda misitu yetu, tunaye shujaa / masifika msomi Wangari ambaye alitunukiwa zawadi ugenini. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuhifadhi mazingira. (alama 4)

(e) Mishororo mine (tarbia) isipokuwa ubeti wa tisa
-beti tisa
-ukaraguni
-lina kibwagizo (Ni wajibu sote kuyalinda mazingira)
-vipande viwili
-Mizani 8, 8 isipokuwa ubeti wa tano mshororo wa kwanza, ubeti wa sita mshororo wa pili na ubeti wa saba mshororo wa kwanza.

(d) Katika shughuli /harakati za kulinda misitu yetu, tunaye shujaa /msifika msomi Wangari ambaye alitunukiwa zawadi ugenini. Ni jukumu la kile mmoja wetu kuhiifadhi mazingira. (alama 4)
(d) (i) Makanda – sehemu
(ii) gwiji – Stadi, hodari, shujaa
(iii) jamali – zuri, bora
(iv) fosi – nguvu, mabavu

(e) Mazida k.v barakatu, kiyoto
- Tabdila k.m Njiya
- Utohozi k.v Nobeli, fosi, profesa, ozoni
- Kuboroga sarufi k.v Ni misitu kuifyeka misitu
- Inkisari k.v Kawa, kaipokea, kaimbiwa, kafika

**-USHA1RI 10**

**-7. Soma utunzi ufuatao halafu ujibu maswali.**

- Piteni jamani, piteni haraka
- Nendeni, nendeni huko mwendako
- Mimi haraka, haraka sina
- Mzigo wangu, mzigo mzito mno
- Na chini sitaki kuweka.
-
- Vijana, kwa nini hampiti?
- Kwa nini mwanicheka kisogo?
- Mzigo nilioubeba haupo kichwani
- Lakini umenipinda mgongo na miguu
- Na lazima nijiegemeze, kichwa chini -nendako.
-
- Haya piteni! piteni haraka ! Heei!
- Mwafikiri mwaniacha nyuma!
- Njia ya maisha ni moja tu.
- Huko mwendako ndiko nilikotoka.
- Na nilipopafika wengi wenu hawatafika.
-
- Kula nimekula na sasa mwasema
- Niko nyuma ya wakati
- Lakini kama mungepita mbele
- Na uso wangu kuutazama
- Ningewaambia siri ya miaka mingi.
-
- (a) Ni mzigo gani unaozungumziwa? Tolea jawabu lako ushahidi. (alamo 3)
- (b) Toa ujumbe unaodokezwa kutokana na mafungu yafuatayo. (alama 4)
- (i) Njia ya maisha ni moja tu. (alama 1) (ii) Kwa nini mwanicheka kisogo? (alama 1) (iii) Huko mwendako ndiko nilikotoka. (alama 1)
- (iv) Na nilipopafikia wengi wenu hawatafika (alama 2)
- (c) Mwandishi (mshairi) anasema kuwa anaweza kuwaambia vijana siri ya miaka mingi.
- Hii ni siri gani? (alama 3)
- (d) Toa ithibati kuwa utunzi huu unaweza kuchukuliwa kuwa ni shairi (alama 6)
- (e) Pendekeza methali zozote mbili zinazodokezwa katika utunzi huu (alama 2)
- (f) Taja na kutoa mifano ya mbinu za lugha katika utunzi huu. (alama 2)

. **USHAIRI JIBU**

a) - Mzigo wa mzee
- Uzito wa maisha – ameyapitia vijana wanayoyapitia.
- Ugumu wa maisha – ni kama mzigo
- Ataka usaidizi – lazima ajiegemeze
- Shida maishani
- Taabu nyingi
- Kulemewa kimaisha. ( zo zote 3 x 1 = 3)

b). - Hali ya maisha ni sawa tu kwa waja wote, ni kama njia na wote tunapitia.
- Kwa nini wacheka ukale wangu, au kwa nini wadharau asili / ukale wangu ?
- Yote mnayopitia sasa mimi nimeshayapitia.
- Kule nimefika hamtafika, wengi wenu hamtafikia umri wa miaka mingi. (4 x 1=4)

c) Siri ya miaka mingi.
- Shida ya maisha

- Maisha ya ujana hadi utu uzima.
- Ujuzi wa maisha kulingana na kuishi kwingi.
- Hajachelewa (nyuma ya wakati) yeye anaenda na wakati. ( zo zote 3 x 1 = 3)

d) - Mizani
- Vuna ( mdundo)
- Beti
- Mistari / mishororo
- Matumizi ya inkisari – mwendako
- Matumizi ya mazida – kuutazama. ( 6 x 1= 6)

e) - Haraka haraka haina baraka.
- Kuishi kwingi ni kuona mengi. (2 x 1 = 2)

f) - Mbinu za lugha
- Balagha – kwa nini humpiti ?...........kisogo ?
- Siyahi – piteni
- Takriri – harakaharaka, piteni, piteni………! ( zo zote 2 x 1= 2)

**USHAIRI 11**

6. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata***.

## HISIA

Ewe hisia!
Umeniamshia ndoto niloisahau zamani
Umelimsha mwangu moyoni
nyimbo ya kale
na mdundo usomvutia
ila hayawani wa mwangu rohoni.

Tulia sasa tulia.
Hebu tulia ewe hisia ulo mtimani.
Nakataa katu kusisimka
kwa sauti yako laini
Kwani njia zetu ni panda
daima hazioani

Umesubutu vipi kuniita
kutoka mwako ngomeni
ulimosahauliwa tangu zamani
Basi yawache maombolezi yako yaso maoni,
yawateke hao mashujaa wa kale
watu walo kaburini.

Hebu tulia, usiniingilie
usinihangaishe!
Kukuandama katu haimkini
Kwani hata sasa…. kwa kukuwaza tu dakika hini
naona majuto ya mbali moyoni
kama kwamba nimegawa wangu wakati
na wazimu, majinuni.
Basi nenda zako hisia…shuu… hebu tokomea.

(a) Huu ni utungo wa aina gani? (Alama 2)
(b) Kwa kutoa mifano fafanua sifa zinazoufanya utungo huu kuwa shairi. (Alama 4)
(c) Eleza mawazo ya mshairi katika shairi hili (Alama 5)
(d) Taja na ueleze mbinu tatu za kifasihi katika shairi hili. (Alama 6)
(e) Andika maneno yafuatayo kwa lugha sanifu (Alama 3)
(i) Niloisahau

(ii) Umesubutu
(iii) Mtimani

**USHAIRI 9**

7. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuatia.***

Sikimbii, Siogopi, hali yangu nachelea.
Sivijui, visa vipi, pale nyuma kutokea
Niendako, sikujui, mkimbizi ninaitwa!

Sitoroki, nchini mwangu, ugenini kutamani
Sidiriki, malimwengu, yananizonga jamani
Niendako, sikijui, usalama nazengea!

Siyajui, nisemayo, machafuzi nayapisha
Siyajui, nionayo, ni maasi ya kutisha
Niendako, sikujui, amani najitakia

Sipotei, sipumbai, hali njema naisaka
Sishangai, sitambui, chanzo cha yangu mashaka
Niendako, sikujui, maskani natafuta.

Afrika, Afrika, wana wako tunalia
Twateseka, twateseka, bara letu kulilia
Kwa majanga, na visanga, ukimbizi kuzidisha.

Viongozi, viongozi, mwongozao Afrika
Mumaizi mumaizi, utulivu kuuweka
Zi nchi zetu, ukimbizi kupunguza.

(a) Lipe kichwa mwafaka shairi hili (Alama 1)
(b) mikondo mitatu ya shairi hili. (Alama 3)
(c) Onyesha mpangilio wa mizani na vina katika ubeti wa tano (Alama 4)
(d) Mshairi ana ushauri gani kwa viongozi wa kiafrika? (Alama 2)
(e) Mshairi ana falsafa gani? (Alama 2)
(f) Taja na ueleze tamathali zozote mbili katika shairi hili (Alama 4)
(g) Shairi la aina hii hutumiwa vipi katika Fasihi simulizi (Alama 2)
(h) Eleza maana ya msamiati huu kwa mujibu wa shairi (Alama 2)
(i) Sidiriki
(ii) Nazengea

**6. (a) (i)** Shairi huru

Sababu – halizingatii arudhi za ushauri k.v urari wa vina, urari wa mizani.
(i) Shairi zohali/zuhali/mtiririko/vue
(ii) Shairi la kimapinduzi

**Kutaja al. 1**
**Sababu al. 1**
**Jumla 2.**

**(b)** (i) Matumizi ya beti
(ii) Matumizi ya tamathali ya takriri
(iii) Matumizi ya mishororo
(iv) Baadhi ya mishororo yaelekea kuwa na vina
(iv)Matumizi ya lugha ya mkato **Zozote 4 x 1 = 4**

**(c) MAWAZO YA MSHAIRI**
(i) Mshairi hataki ndoto za zamani ziamshwe

(ii) Hataki kuibuliwa kwa kumbukumbu za mambo ya kikatili /kihayawani
(iii) Akataa kukumbushwa hisia za yaliyopita
(iv) Hataki kuangaishwa na hizo hisia
(v) Hizi hisia zamdhulumu / zamdhuru / zina athari mbaya kwake.
(vi) Akataa katakata kuzipokea hizo hisia **Zozote 5 x 1 = 5**

**(d) mbinu za kifasihi**
(i) nidaa – Ewe hisia!
(ii) tashhisi – hisia
(i) sitiari – ndoto, hisia
(ii) takriri –tulia sasa tulia,hebu tulia
(iii) mbalagha-umesubutu vipi kumuita……..?
(iv) mdokezo – basi nenda zako hisia ……..
(v) tashbihi – majuto ya mbali moyoni kama kwamba…………
**zozote 3x2 = 6 kila mbinu ifafanuliwe**

**(e)** Niloisahau – niliyosahau
Umesubutu – umedhubutu
Mtimani – moyoni **3x1**
7. (a) Mkimbizi
(b) (i) Tathlitha – mishororo mitatu kila ubeti
(ii) Ukawafi – vina (vipande) vitatu kila ubeti
(iii)Ukaraguni – vina vya keti na vya mwisho vinahitilafiana.

(c) Mizani 4, 4, 8
4, 4, 8
4, 4, 8 1 x 2 = 2
Vina ka, ka, a,
ka, ka, a,
nga, nga, sha 1 x 2 = 2

(d) Viongozi wa kiafrika wanafaa kutanabahi na kuweka utulivu / amani katika nchi zetu ili ukimbizi upungue.
**1 x 2 = 2**
(e) Falsafa / msimamo wa mshairi ni kuwa hakuna haja ya watu barani Afrika kuwa wakimbizi bila sababu za maana. Alama 2.

(f) (i) Takriri – msisitizo wa ujumbe fulani .
Maneno mengi na silabi 'si' ya ukatavu imetumiwa kusisitiza ujumbe – kukataa ukimbizi.
(ii)Ritifaa ' zi' ufupisho wa maneno.
(iii)Nidaa (mshangao) – kiitikio cha ubeti wa kwanza na wa pili. (2 x 2 = 4)
(g) Utunzi wa nyimbo hasa za taarabu baina ya jamii za pwani. Huwaongoa wanajamii katika sherehe mbali mbali na kuwatuliza 1 x 2 = 2
(h) Sidiriki – siwezi
Nazengea – natafuta 2 x 1 =2

**USHAIRI 12**
**1. Soma shairi hili kisha ujibu maswali.**

Jicho, tavumiliaje, kwa hayo uyaonayo?
Kicho, utasubirije, maonevu yapitayo
Kwacho, lijalo na lije, nimechoka vumiliyo

Naandika!

Moyo, unao timbuko, maudhi tuyasikiayo
Nayo, visa na mauko, wanyonge wayakutayo
Kwayo, sina zuiliko, natoa niyahisiyo
Naandika!

Hawa, wanotulimiya, dhiki wavumiliayo
Hawa, mamiya mamiya, na mali wazalishayo
Hawa, ndo wanaoumiya, na maafa wakutayo
Naandika!

Hawa, sioni wengine, kwao liko angamiyo
Hawa, uwapa unene, watukufu wenye nayo
Hawa, bado ni wavune, kwa shida waikutayo
Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo
Bado, tafauti sana, kwa pato na mengineyo
Bado, tuling'owe shina, ulaji pia na choyo
Naandika!

**Maswali**

(a) Shairi hili laweza kuwekwa katika bahari zipi? (alama 4)
Thibitisha kila jibu lako.
(b) Eleza dhamira ya mshairi. (alama 2)
(c) Onyesha mifano miwili ya uhuru wa kishairi jinsi ulivyotumika katika shairi. (alama 2)
(d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 4)
(e) Tambulisha kwa mifano mbinu zozote mbili za sanaa katika shairi. (alama2)
(f) Fafanua sifa za kiarudhi zilizotumika katika ubeti wa tano. (alama 3)
(g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 3)
(i) Zuiliko
(ii) Wavune
(iii) Wenye pupa na Kamiyo.

1.a)**Tarbia** - Lina mishororo minne katika kila ubeti
**Msuko -** Kibwagizo kimefupishwa.
**Ukara-** Vina vya nje vinatiririka katika beti zote ilhali vya ndani havitiririki.
**Ukawafi-**Una vipande vitatu (ukwapi, utao na mwandamizi) katika mishiroro ya kwanza mitatu ya kila ubeti isipokuwa kibwagizo
**Kikwamba** – Katika beti za 3-5 neno moja ndilo linaanza kila mshororo.
**Sakarani** – Kuna bahari kadhaa katika shairi. ***Zozote 4 x 1 = 4***

b) Kuwahimiza watu (hasa wanyonge ) wainuke na kupinga maovu na maonevu wanayofanyiwa na matajiri wenye uwezo. ***1 x 2 = 2***

c) Inkisari km vumiliyo – kuvumilia nanaandika.
Mazida kurefusha k.m. angamiyo, vumiliyo n.k.
Tabdila k.m mamiya badala ya mamia ***Zozote 2 x 1 = 2***

d) Hawa wanaotulimia wanavumilia dhiki
Wao ni wengi na ndio huzalisha mali.
Wao ndio wanaoumia na kupata mateso / taabu
Wanayokumbana nayo.Ninaandika / ninasema ***Zozote 4 x 1 = 4***

e) **Takriri** – hawa, bado, mamiya.
**Balagha** – uyaonaje?

**Taharuki** – Naandika!
**Inkisari** – Hawa, ndo
**Kinaya** – Watukufu wenye nayo ***Zozote 2 x 1= 2***

f) Kuna mishororo minne

Kuna vipande vitatu katika mishororo ya kwanza mitatu na kimoja katika kibwagizo

Vina vinatiririka / vinafanana

**Mizani** 2,- 6-8
2-6-8
2 – 6 – 8
4 ***Zozote 3 x 1= 3***

g) i) Cha kunizuia / kizuizi / kizingiti / uoga / hofu/ pingamizi

ii) Wachovu /dhaifu /hafifu

iii) Walio na tamaa kubwa / walafi/ mabwanyenye

***3 x 1 = 3***